Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao, na kwa yakini Atawaimari-shia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na cho chote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri. ***(An-Nuur 24:56).***

JUZU 73 No. 169 | RAMADHAN 1433 AH | AGOSTI 2012 | ZAHOOR 1391 HS | BEI TSH. 500/=

Kiongozi wa waaminio duniani amuonya Obama:

Vita ya Tatu ya dunia yanukia

Na Mwandishi Wetu

Kufuatia hali inayotishia amani ya dunia, Kiongozi wa waaminio duniani hadhrat Mirza masroor Ahmad a.t.b.a. amemuandikia barua Rais wa Marekani Barak Hussein Obama ya kumkumbusha nafasi ya Marekani katika kudumisha amani duniani. Ifuatayo ni barua hiyo ya Kiongozi wa kiroho kwa kiongozi wa taifa lenye nguvu duniani.

Rais Barak Obama!

Kufuatia tufani katika bahari ya kisiasa duniani, nimeona ninao wajibu mkubwa wa kukuandikia wewe rais wa Marekani, nchi ambayo ina nguvu kuliko zote duniani, kwani ni dhahiri shahiri ya kwamba unao uwezo na mamlaka ya kufanya uamuzi ambao utakuwa na athari sio tu nchini kwako bali duniani kote.



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a.



Barak Obama, Rais wa Marekani

Kwa hivi sasa kuna wasiwasi na taharuki kubwa duniani. Vita inaendelea katika baadhi ya sehemu sehemu duniani. Kwa bahati mbaya mataifa makubwa duniani hayajafanikiwa kama ilivyotarajiwa kuleta amani palipo na vita.

Duniani kote tunachokiona kwa hivi sasa ni kwamba kila nchi inaunga mkono au inapinga mwenendo wa nchi nyingine. Haki haitendeki hata kidogo. Tukitazama hali halisi ilivyo kwa hivi sasa hapana shaka jiwe la msingi la vita kuu nyingine ya dunia limekwisha wekwa. Nchi kubwa na ndogo kwa hivi sasa zina silaha za kemikali na hivyo kuongeza malalamiko na uhasama. Kaitka hali hiyo ni wazi ya kwamba

Endelea uk. 2

Ukhalifa katika Islam

Na Mwandishi wetu,
Dar es Salaam

Ndugu na Jamaa, wake kwa waume na wakubwa kwa watoto, leo ni siku ya Ukhalifa. Siku hii ni muhimu sana kwa Waahmadiyya walio katika kila taifa. Inatukumbusha tukio la miaka 104 iliyopita ambapo Mwanajumuiyya wa kwanza kufanya Baiat siku hiyo Maulvi Hakim Nuruddin alichaguliwa kuwa Khalifa. Ni zaidi ya Karne moja sasa. Ukhalifa wetu umeendelea kuishi, kunawiri na kuchanua ukiyashinda majaribu yote yaliyoelekea kusababisha maafa. Hili halikutokana na ujanja wetu, uhodari wa mbinu au uwingi wa maarifa. Bali ni kutokana na mapendeleo ya Allah ndiye muasisi wa hii falsafa.

Bila shaka Ukhalifa ni muhimu muhimu kwa ajili ya uhai wa imani na ndio mwamvuli ambao Allah huutumia kusitiri waja wake. Ndiyo maana tunaona ya kwamba hata nabii wa kwanza, Adam a.s., alipotumwa duniani alifanywa kuwa Khalifa wa kaumu yake. Mola wetu hakufanya hivyo kwa ajali ya bahati nasibu, bali ulikuwa ni mpango maalum ambao Yeye Mwenyewe Aliijua hekima yake. Mwenyezi Mungu Alijua kuwa nje ya nidhamu ya Ukhalifa mwanadamu anaweza kuwa ayari mkubwa juu ya maisha ya wenzake na hata juu ya maisha yake. Ndiyo maana kila alipoletwa Nabii kufanya mageuzi ya kiroho kwa jamii nidhamu ya Ukhalifa ilisimikwa mara tu baada mauti yake.

Ni ukweli ulio wazi kwamba msiba wa Nabii utokeapo dunia hufikwa na simanzi isiyo pata kuwako. Hii ndiyo hali iliyowakuta Masahaba wa Mtume (saw) katika siku ambayo alifikwa na mauti. Kuna waliohisi kuwa kwa kifo chake, dini aliyoiasisi haitaendelea kupata mashiko. Katika uwanja wa msiba pale Masjid Nabawiy nyuso zote zilionekana kuelemewa na huzuni na masikitiko. Wakati huo maadui wa Islam walikuwa wakivinjari na kutaanasa wakisherehesha dhifa zao kwa tabasamu na vicheko. Waliamini kuwa msiba huo ulikuwa ndiyo mwisho wa mahubiri ya Islam ambayo wao kwa muono wao yalikuwa ni mazalia ya fitina na choko choko.

Hadhrat Ummar Bin Khattab (ra) alishindwa kabisa kuhimili uzito wa msiba huu. Alihisi kwamba kama iachwe ijulikane juu ya kifo cha Mtume (saw) bila shaka dunia itaingia katika simanzi kuu. Aliamua kupiga marufuku mtu yeyote kutangaza umauti wa Nabii huyu, aliye bora na mkuu. Alitishia kumfyeka kwa upanga wa shingo mtu yeyote atakaye tangtaza kufa kwa Mtume (saw) hata kama ni kwa kunukuu. Ingawa Hadhrat Ummar (ra) alionekana kama mtu aliyechanganyikiwa kutokana na huzuni ya hali ya juu, lakini alifanikiwa kudhibiti hali kwa kuepusha baadhi ya masahaba kujisahau na kupiga ukelele kwa vilio vikuu. Naam! Ndivyo ilivyokuwa kwa maana kutokana na amri yake masahaba wote walioonekana kulialia na kuomboleza wakinyamaza kimya, tena ghafla bin vuu.

Ndipo tukio likachukuliwa na mtu mtawa kuliko wote aliyejaa nuru ya haki. Huyu alikuwa ni Abdullah mwana wa Abi Kahafa (ra) aliyejulikana sana kwa lakabu yake Abubakar Siddiq. Alikuwa ni mtu mwenye haiba kubwa na uhodari mpevu wa kumiliki mikiki. Huyu ndiye aliyemudu kutoa tangazo rasmi la kifo hicho tena kwa kutumia hoja za

Endelea uk. 2

Kikombe cha 'Babu'kiko wapi?

Neno la Yesu Kristo lilikuwa nguvu ya soda?

Na Pazi Kitabu Mazongera

"Kinachotibu siyo haya maji na dawa iliyomo kwenye hiki kikombe bali ni neno la Yesu lililomo kwenye haya maji ambayo yemebarikiwa na kristo". Haya ni baadhi ya maneno aliyoyatoa Mchungaji Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Ambilikile Mwasapile (76) maarufu kwa jina la 'Babu' wakati akihojiwa na Mtangazaji wa Shirika la Utangazaji la BBC la nchini Uingereza katika kijiji cha Samunge Wilaya ya Loliondo. Alisema ameoteshwa dawa hiyo na Roho Mtakatifu mwaka 1991, ambayo gharama yake ilikuwa ni shilingi mia tano na ni marufuku kurudia.
Tunakumbuka namna Serikali ilivyoelekeza nguvu zake hadi kufikia Waziri wa nchi ofisi ya Waziri Mkuu anaeshughulika na Sera na uratibu wa Bunge Mh. William Lukuvi kutoa maelekezo mahsusi namna ya kufanya ukarabati wa barabara ya kwenda kwa 'babu' ikiwa ni pamoja na mipango ya dharura ya kujenga madaraja yaliyokuwa mabovu. Huku akiahidi msaada wa hali na mali katika kumsaidia 'Babu' kutekeleza majukumu yake bila ya matatizo. Mamia kwa mamia ya watu walikuwa wakimiminika Loliondo kwa imani kwamba neno la Yesu Kristo lililomo kwenye dawa ya 'babu' kweli ni kiboko cha maradhi mengi yasiyotibika kwenye mwili wa binadamu. Aidha tunakumbuka gharama ya usafiri ya kwenda Semunge ilivyopanda ghafla ambako ni umbali wa kilometa mia nne toka Arusha Mjini. Kuanzia Mawaziri, Wabunge, Madiwani, Wafanyabiashara, Matajiri na maelfu

Endelea uk. 3

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Tutasahu hadi lini?

Moja ya tatizo letu kama taifa ni kusahau. Tumeyasahau yale amabayo hatutakiwi kuyasahau, na kuyakumbuka yale ambayo hayatuongezei mkate wala shibe.

Siku za mwanzo za uhuru wetu tuliambizana kinagaubaga tuache majikogo na kwamba tujitahidi tushone koti letu sawa na kitambaa tulicho nacho. Tulikumbushana tusijifanye hamnazo kwa kujitia ufahari kana kwamba sisi ni watoto wa mfalme ilhali tuko taabani mithili ya chaupele tukijikuna tunatoa unga.

Somo hili tulilielewa, lakini waliyoelewa zaidi ni viongozi wetu. Fahari za kipuuzi zikaondolewa. Mikutano ya asubuhi na jioni ikapunguzwa. Gari za kawaida zikanunuliwa kwa viongozi wetu. Idadi ya watu katika ujumbe ikapunguzwa. Viongozi wakaonesha uchungu mkubwa kwa kila senti iliyotoka na ikahakikishwa kuwa imetumika ki halali.

Kweli majira sasa yamebadilika. Ni wachache ambao wana maumivu ya nchi hii katika nyoyo zao. Ni wachache wanaojali tnakoelekea. Hizi ni enzi za ponda mali kufa kwaja. Tumbua hujui kesho itakuwaje. Na utamaduni huu unaendelea kwa kasi kubwa kwa sababu watu wanajiuliza je hawa waliofuja mali ya uma wamefanywa nini? Sasa ni wakati wa aliye nacho kuongezewa zaidi, sasa ni safari zisizokwisha. Magari ya kifahari, kwenye donda tunazidi kuweka msumari wa moto.

Kana kwamba hiyo haitoshi, tunaambiwa kuwa ndege ya kifahari ya rais itanunuliwa hata kama kufanya hivyo itatubidi tule majani. Ndege ni bora kuliko binadamu. Na hii ni kinyume kabisa na itikadi tuliyoanza nayo ambayo ilimpa utukufu binadamu kuliko kitu chochote kile. Hali hii kwa bahati mbaya imeenea katika bara zima la Afrika. Afrika iliyotafuta uhuru ili ipate maendeleo sasa hivi imo katika maumivu makubwa.

Na hivi karibuni zimetolewa takwimu zinazoonyesha jinsi gani pesa za wakulima na wafanyakazi wa nchi hii zimewekwa katika mabenki ya Uswizi kwa ajili ya watu wachache. Huo ni ubinafsi na ni jambo la kuumiza moyo. Matatizo tuliyonayo hapa nchini, mashuleni, mahospitalini, ni matatizo ambayo kila mwenye senti yake nje angeweza kuirudisha nchini ili isaidie kuleta maendeleo katika jamii yetu. Nia hasa na furaha ya kupata uhuru ilikuwa ni kupata maendeleo na kuhakikisha ya kwamba tunayasema yale tunayoyatenda.

Furaha yetu ilikuwa kubwa mno tulipopata taarifa ya kwamba kuna baadhi ya viongozi wa Afrika ambao wanaanza kupona. Bi. Joyce Banda Rais wa Malawi inaonesha amekuwa wa kwanza kupona. Kwa ujasiri mkubwa ameagiza magari yote ya kifahari yasitumike na ndege ya kifahari ya rais iwekwe kando.

Malawi siyo mbali kutoka kwetu. Tumekuwa na uhusiano wa karibu na nchi hiyo. Kamuzu Banda hapa palikuwa nyumbani kwake. Na waziri wake wa mambo ya nchi za nje Kanyama Chiume tulikuwa nae katika mapambano ya uhuru. Hivyo sisi watanzania tuna haki ya kuelewa kwa haraka aliyoyafanya Bi. Joyce Banda. Tufanye haraka kujifunza kutoka kwa nchi hiyo jirani ili tuweze kuwapunguzia mzigo wakulima na wafanyakazi wa nchi hii ambao wameendelea kuumia na kuteseka wakati nchi yao imejaaliwa kuwa na vigezo vyote vya kuleta maendeleo.

Wakati huo huo kwa unyenyekevu mkubwa tunamshukuru Allah aliyempatia rais wetu hekima na busara ya kuchagua meza ya mazungumzo badala ya vita kuhusu mgogoro wa ziwa Nyasa (Malawi) baina yetu na majirani zetu. Allah dawamu yupo na wale wanaosimamisha amani. Mungu Ibariki Tanzania Mungu Ibariki Afrika.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Kiongozi wa waaminio Amuonya Rais wa Marekani

Kutoka uk. 1

vita kuu ya tatu ya dunia inanukia. Vita hiyo bila shaka zitatumika silaha za hatari ambazo zitaleta maangamizo makubwa sana. Kama njia ya usawa na haki ingefuatwa toka vita kuu ya pili 1939 - 1945 tusingelikuwa tunaona hali ambayo imejitokeza ambayo ina dalili zote za vita.

Kama sote tunavyoelewa chimbuko hasa la vita kuu ya pili ya dunia, lilitokana na kushindwa kwa *Legue of Nations* na mtibuko wa uchumi ulioanza mwaka 1932. Hali hii ya uchumi tulio nayo wakati huu inashabihiana na ile ya mwaka 1932. Tunaona matatizo ya kisiasa na kiuchumi yameelekeza kwenye vita katika nchi changa na pamejitokeza mtafaruku katika nchi hizo. Hali hii ina uwezekano mkubwa kutupeleka kwenye vita kuu ya dunia. Kama matatizo na uhasama havitamalizwa kwenye meza ya mazungumzo na diplomasia, hii itapelekea katika kuanzishwa kambi za uhasama miongoni mwa mataifa. Bila shaka hatua hii itakuwa kichocheo kikubwa cha kuanzishwa kwa vita kuu ya tatu ya dunia.

Hivyo ninaamini kwamba kwa hivi sasa badala ya kutoa kipaumbele kwa maendeleo ya dunia, ingelifaa na ninadhani ni jambo la lazima kuongeza juhudi ili kuinusuru dunia kutoka kwenye maangamizi. Kuna haja ya haraka sana kwa binadamu kumtambua Allah, ambaye ni muumba wetu, kwani hiyo ndio njia pekee ya kuhakikisha kuwa kuna amani duniani. Bila mwelekeo huo dunia inaelekea kwenye maanguko ya kutisha.

Ombi langu kwako, kwa hakika kwa viongozi wote duniani ni kwamba badala ya kutumia nguvu katika kukandamiza mataifa mengine, inafaa kutumia diplomasia, mazungumzo na hekima. Mataifa makubwa duniani kama vile Marekani, lazima yatimize wajibu wake wa kuleta amani duniani. Wasiendekeze mwenendo wa nchi changa kama kisingizio cha kuchafua amani ya dunia.

Hali tuliyo nayo ni kwamba, silaha za maangamizi zimo mikononi mwa mataifa makubwa na baadhi ya mataifa madogo. Na mara nyingi walio madarakani ni viongozi wasiothamini maisha ya watu. Hivyo ni ombi langu kuwa ujitahidi kuyaepusha mataifa makubwa na madogo yasitumbukie katika vita vya tatu. Hakuna wasiwasi wowote kuwa tukishindwa katika jukumu hili, maafa hayo hayatakumba nchi maskini za Afrika, Asia na Marekani ya kusini tu, bali vizazi vijavyo navyo vitaathirika sana. Na watoto wengi duniani watazaliwa na ulemavu. Watoto hao hawatawasamehe hao walioruhusu hali hiyo itokee. Badala ya kufikiria maslahi yetu tu, inatubidi tufikirie kizazi kijacho na kuwatengenezea maisha yenye matumaini.

Namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu Akujaalie wewe na viongozi wote duniani kuelewa ujumbe huu.

Umuhimu wa Ukhalifa

Kutoka uk. 1

kimantiki. Baada ya maliwazo yake, waumini wakaliwazika na hoja zake zilimfanya hata Ummar apunguze hamaki.

Hata kama Ummar (ra) alipinga umauti wa Mtume (saw) lakini bila shaka alitoa bishara ya haki. Ni bishara iliyoonyesha utimilifu wake kuanzia wakati ule hadi katika kizazi hiki. Madai yake ni kwamba Mtume (saw) kamwe hajafariki dunia. Bali amekwenda kupokea amri tu kwa Muumba wake na siku zijazo atarejea. Ukhalifa wa Abu Bakar (ra) uliifanya bishara hii kutimia chini ya Ukhalifa wake Islam iliwashinda wapinzani na kuwarudisha kundini baadhi ya wale walioikimbia. Katika uhai wa Khilafat Rashida (Ukhalifa ulioongoka) ni kana kwamba uhai wa Muhammad (saw) ulijirudia. Hata baada ya Ukhalifa ule kugawanyika bado Waislam waliendelea kuitawala dunia, baada ya Waislam kupoteza kabisa dira ya Ukhalifa ndipo zikaja zama Ukhalifa wa Kiahmadiyya. Bila shaka huu ni ujio wa pili wa Mtume (saw) ambao kwa vyovyote Hadhrat Ummar katika madai yake alikuwa akiurejea.

Ni kweli Hadhrat Muhammad Mustafa (saw) anatajwa kurudi mara ya pili katika aya hii "WA -AKHRARIINA MINHUM ....." (62:3). Hapa panatajwa juu ya ujio wa Buruuz (Kivuli) wa Muhammad (saw) ambaye atakuwa Nabii. Ukhalifa aliouasisi mtu huyu unaendelea kuwepo hadi leo hii. Bila shaka yoyote Ukhalifa huu ndio unaoishikilia amani ya dunia.
Historia inao ushahidi wa kutosha ya kuwa wakati wowote Waislam walipokosa Khalifa waliishi kwa shida na taharuki. Waislam walitawaliwa, walinyonywa, walinyanyaswa na kunyimwa haki. Wakati fulani waliuawa kwa kuchinjwa si kwa maelfu bali kwa malaki. Ulipoanguka Ukhalifa wa Kiumayya katika Baghdad idadi ya Waislamu waliochinjwa kwa siku moja ilikaribiana mno na idadi ya walokufa katika mauaji ya halaiki. Hali hii ilitokea tena katika Hispania pindi Ukhalifa wa Waislam ulipoangushwa na watawala wa Kikatoliki.

Haya ni sehemu tu ya matukio mengi yanayoonyesha umuhimu wa Khilafat kuwepo kwa Waislam katika kila wakati. Ni Khalifa tu duniani ndiye anayeweza kuhesabika kuwa kiongozi wa dhati. Kama tuonavyo kwamba hata mtaa tu ukosapo uongozi maisha huwa ni ya hati hati. Mauaji ya kimbari yaliyotokea Rwanda na hali ilivyo sasa katika Somalia ni shuhuda za nukusi za kukosa uongozi zisizohitaji utafiti. Maafa hayo yaliwakumba watu wa nchi hizo baada ya kupitisha muda mfupi tu bila ya kuwa na mwenye kiti. Ndiyo maana katika Dola mbalimbali, gharama na nguvu kubwa hutumika kuwalinda wafalme, maraisi na wenyeviti.

Ikiwa huu ndio uharibifu uliotokea katika nchi moja moja kwa kukosa uongozi basi hali itakuwaje kwa dini ya dunia nzima ikosapo uongozi kwa karne kadhaa. Ndiyo maana Waislamu wengi walio nje ya Ukhalifa kila wakati hushikwa fadhaa. Imefikia hatua ya wao kushindwa kuhubiri amani ambayo ndiyo ujumbe rasmi wa Islam na badala yake wamegeuka kuwa mahodari wa kuzua mabalaa. Ugaidi, uuaji, mapinduzi, mapigano na maandamano ya fujo ndiyo mambo wanayodhani kuwa yatawafaa. Kila mtu na Lwake, kati yao hakuna mtu anayeweza kutamka kuwa Waislamu kaeni kisha wakakaa. Ni sisi Waahmadiyya tu ndilo kundi lenye mtu ambaye akiamuru hakuna atakayekataa.

Ikumbukwe kwamba Ukhalifa tulio nao haukusimikwa kwa juhudi za wanaharakati. Ni fadhila tu ambazo Allah Amezishusha kwa ajili ya huu umati. Ni matokeo ya shukurani za Masahaba ambao hawakuridhia kufanya usaliti. Kila alipopatikana Khalifa hawakukengeuka isipokuwa walimtii kwa kufanya naye Baiat.

Aya aliyoisoma Hadhrat Abubakar (ra) akithibitisha kifo cha Mtume (saw) (3:145) inaishia na maneno haya. "WASAJIZI LLAAHUSH - SHAAKIRIIN" malipo ambayo Allah Aliwalipa wanaoshukuru ni Ukhalifa ambao kuupata ni bahati. Kumwabudu Allah bila kumshirikisha na chochote katika kuulinda Ukhalifa limetajwa kama sharti.

Chonde chonde ndugu zangu tuliofanya Baiat na Khalifa wa Allah hatuna budi kuonyesha utii wa dhati. Kumtii Khalifa ni kutii kila kiongozi aliyewekwa kwa nidhamu ya Jamaat. Tuonyeshe utii bila kuangalia kuwa kiongozi aliyewekwa na nidhamu hii ni wa kabila gani au taifa gani. Ewe Ahmadiyya muombe sana Mola wako ili akupe utii usio na eti eti. Na kama moyo wako utakushawishi kuvunja utii basi tafadhali ukomeshe haraka mithili ya Mshairi nguli Khamisi Sultani Shamte Wamwera anavyoukomesha moyo wake kwa kuuambia "***koma moyo wangu koma, koma ja mkoma titi***".

Mwl. Labandin Amani ametutoka duniani

Na Mwl. Abdullatif Y. Ngarombe - Mkuyuni, Morogoro

Mnamo tarehe 13/06/2012 siku ya Jumatano ilikuwa ni siku ya huzuni kwani Mwalimu wetu kipenzi Labandin Amani Lukalango alifariki dunia katika muda wa saa 1:30 jioni katika Hospitali ya Mkoa wa Morogoro. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tunarejea.

Marehemu aliugua kwa muda mfupi maradhi yaliyopelekea kifo chake ambayo yalimuanzia Morogoro Mjini alipokwenda kushiriki Mkutano wa Jalsa ya Mkoa huo wa Morogoro. Mkutano huo ulifanyika tarehe 01 - 02/06/2012 katika siku za Ijumaa na Jumamosi katika viwanja vya Jamaat huko Kihonda Morogoro.

Siku ya Jumamosi tarehe 02/06/2012 saa nane mchana Marehemu alitoka Msikitini alikokuwa amejipumzisha na kuanza kutembea barabarani akiwa anakokwenda hakujulikani. Mkewe marehemu alijaribu kumfuatilia na kumuuliza anakokwenda, lakini hakuweza kumjibu chochote. Ndipo mke wa marehemu akaja kutoa taarifa kwa Walimu wa Morogoro kwamba marehemu mume wake amechanganyikiwa na alikuwa anaongea maneno yasiyoeleweka. Walimu kwa pamoja tuliungana na mke wa marehemu katika kumtafuta Mwalimu Labandin.

Baada ya kumtafuta kwa muda mrefu ndipo tukamkuta maeneo ya Bima Kihonda Magorofani karibu na barabara kuu iendayo Dodoma, umbali wa takribani kilometa 2 kutoka Msikitini alikokuwa amepumzika. Tukamchukua Mwalimu garini na kumkimbizia hospitalini, kule hospitalini alipokelewa vizuri na alipatiwa kitanda ambako alilazwa kwa muda wa siku tano na hali yake ilionekana inaendelea vyema, kwani alikuwa anaongea kama kawaida na madaktari wake waliamua kumruhusu kurudi nyumbani. Hivyo tarehe 07/06/2012 Alhamisi Mwalimu alirudishwa kwenye kituo chake cha kazi - Duthumi yeye pamoja na familia yake.

Usiku wa tarehe 10 Jumapili Mwalimu hali yake ilibadilika tena huko Duthumi. Kulingana na hali ya mgonjwa ilivyokuwa iliwalazimu wauguzi wa hospitali ya Kijiji -Duthumi kutoa gari lao maalum la kubebea wagonjwa (Ambulance) na kumchukua Mwalimu hadi Morogoro Mjini kwenye hospitali kubwa ya Mkoa alikokuwa



Mwl. Labandin Amani

amelazwa mara ya kwanza. Na ikatokezea kuwa akalazwa tena kwenye wodi ile ile ya mara ya kwanza - wodi tisa.

Kutoka Duthumi mjumbe mmoja wa Jamaat ambaye ni Katibu wa Jamaat ya Duthumi Bw. Twahir Mnungu. Hapo hospitalini Mwalimu Labandin aliendelea na matibabu. Madaktari wake walijitahidi kumpatia matibabu, lakini kwa kudura za Allah ilipofika siku ya Jumatano saa 1:30 jioni Mwalimu Labandin akafariki dunia. Inna lillahi wa inna ilaihi rajiun. Madaktari walieleza kuwa Marehemu alikuwa anasumbuliwa na malaria kali, pia alikuwa anasumbuliwa na fangasi ambayo iliingia kwenye damu.

Marehemu alizaliwa mwaka 1972 mkoani Rukwa katika Wilaya ya Mpanda. Na alijiunga na Jumuiyya mwaka 1991 kwa kuhubiriwa na Mzee Omari Sebuge wa Mpanda. Katika familia yao ni yeye na baba yake pamoja na watoto wawili wa kaka yake ndio waliobahatika kujiunga na Jamaat Ahmadiyya.

UTUMISHI WAKE KATIKA JAMAAT

Marehemu alipata bahati ya kusoma katika chuo cha ubashiri cha Jamia Ahmadiyya huko Morogoro katika mwaka 1996 na alipohitimu masomo yake, Mwalimu alipangiwa kazi ya Ualimu wa Jamaat na kituo chake cha kwanza kilikuwa ni Dodoma. Baadae Mwalimu alihamishiwa katika Jamaat ya Izazi huko mkoani Iringa kabla ya kupelekwa katika Jamaat ya Mtibwa huko Turiani Mkoani Morogoro. Hatimaye Mwalimu alihamishiwa kwenye Jamaat ya Duthumi mkoani humo humo Morogoro ambako aliendelea kuitumikia Jamaat mpaka alipopatwa na mauti.

TABIA NA KHULKA YA MAREHEMU

Mwalimu alikuwa na tabia ya upole sana na mkimya, lakini wale waliopata bahati ya kukaa pamoja nae waliweza kushuhudia kipaji chake cha hali ya juu cha mahubiri kwa uchambuzi wa ndani zaidi wa aya mbalimbali na mahala zinapopatikana kwa kumbukumbu ya kichwa.

SHUKRANI

Shukrani kwa Amir sahib na Mbashiri Mkuu, pia Mbashiri wa Mkoa wa Morogoro ambao walitoa kila kilichotakiwa hospitalini hapo katika kuhakikisha wananusuru maisha ya Marehemu, lakini Allah Alikwishapanga utaratibu mwingine kuhusu maisha ya Mwalimu. Pia shukrani zingine ziwaendee Mkuu wa chuo Jamia Ahmadiyya na Masheikh wote wa Morogoro, Waalimu wote wa Morogoro na Wanajumuiyya wote wa Morogoro ambao walishiriki kwa namna moja ama nyingine katika kumsaidia marehemu Mwalimu Labandin Amani. Na tunamuomba Allah Awalipe malipo mema. Amin

MAZIKO

Marehemu alizikwa kwenye makaburi ya watu wa Wasia yaliyoko Dar es salaam, Wailes Temeke. Mazishi yake yalifanyika siku ya Alhamisi tarehe 14/06/2012 saa 11 jioni. Mwenyezi Mungu Aiweke roho ya marehemu Mwalimu Labandin Amani Lukalango mahala pema peponi. Amin

Kikombe cha 'Babu' kiko wapi?

Kutoka uk. 1

ya watu wa kawaida walienda Semunge kwa 'Babu' na wakati mwingine kwa ufadhili wa watu mbalimbali wenye uwezo wa kuwasafirisha. Wako Wabunge waliowasafirisha wapiga kura w ao waliohitaji huduma ya 'Babu' kwa gharama zao na misafara ya magari ilikuwa haina mfano na ghafla kijiji kilipata wahamiaji wa ndani na nje ya nchi. Aliyekuwa Waziri wa Mali Asili na Utalii, Ezekiel Maige, Waziri wa Ujenzi Dr. John Pombe Magufuli, Waziri wa nchi Ofisi ya Makamu wa Rais aneshughulika na Mazingira, Dr. Teresya Huvisa. Hao ni miongoni mwa Mawaziri waliotangazwa wakipata kikombe cha 'babu'. Wako wagonjwa waliotoroka au kuomba ruhusa katika hospitali nyingi nchini kwenda kwa 'Babu' kwa ajili ya kupata kikombe. Alisikika pia Waziri Mkuu Mizengo Kayanza Peter Pinda akitoa maelekezo bungeni namna ya kufanya watu wanaokwenda Semunge hawapati adha ya usafiri ikiwa na kupata huduma ya kwanza wakiwa kwenye foleni ya kuingia Semunge. Kwa ujumla tulifika mahala kila chombo cha habari ni lazima kitoe taarifa ya 'Babu' ili kiweze kufanya biashara.

Hali imekuwa tofauti kadiri siku zinavyozidi kwenda kwani hivi karibuni wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, wameitaka Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kumfungia Mchungaji Ambilikile Mwasapile kutoa huduma kwa madai kwamba amekuwa akisababisha vifo vingi tangu alipotangaza dawa yake.

Walidai 'Babu' alipotangaza kutibu magonjwa sugu matano, kikiwamo Kisukari, Pumu, Kansa, Kifua Kikuu na Ukimwi, wagonjwa wengi walishawishika na kutoka hospitalini kwenda kupata kikombe chake. Walisema Waheshimiwa Wabunge kuwa matokeo yake vifo vingi vimetokea, hivyo wakaihoji TFDA sababu ya kutomsimamisha 'Babu' kuendelea kutoa huduma yake.

Hoja hiyo iliibuliwa na Mbunge wa Chaani (CCM), Alli Juma Haji, ambaye alisema 'Babu' amekuwa akiwaumiza watu, hivyo akashauri kusimamishwa kwa huduma yake ili kuondokana na tatizo hilo.

Hoja hiyo iliungwa mkono na Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zarina Madabida. Alisema 'Babu' alitangaza kutibu magonjwa makubwa na dunia nzima ilishamjua anayatibu, lakini tayari watu wengi wamekwisha kufa kwa kuacha dawa za hospitali.

Akijibu hoja hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Dawa na Vipodozi, Mitangu Fimbo, alisema TFDA haitoi vibali vya dawa kama anazotumia 'Babu' kutibu.

Fimbo alisema vibali vya dawa za aina hiyo hutolewa na Baraza la Dawa Asilia. Alisema kazi ya kumchunguza 'Babu' hadi kusi-



Babu akigawa Kikombe kwa viongozi!

mamishwa inaweza kuchukua mwaka mmoja.

Fimbo alisema kwa sasa wanaendelea na uchunguzi ili kubaini tatizo hilo na kwamba, katika uchunguzi huo wanashirikiana na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) pamoja na tume ya Sayansi na Teknolojia.

Alisema utafiti huo unasimamiwa na NIMR na kwamba, utakapokamilika , majibu yatatolewa na wananchi watapewa taarifa. Aliyekuwa Naibu Waziri wa Afya, Dk. Lucy Nkya kupitia mahojiano na Mchungaji huyo katika Televisheni ya Taifa, TBC, anasema - Serikali inafuatilia dawa zake na kwa kuwa ni za miti shamba zitachunguzwa, zikithibitishwa kwamba hazina madhara kwa watumiaji haziwezi kuzuiwa. Naibu Waziri akawaonya wagonjwa wanaopata matibabu ya HIV dhidi ya kuacha kutumia matibabu ya kitalaamu.

Katika kikao kimoja cha bunge Wabunge kadhaa waliendelea kuhoji kwa Serikali kuchukua muda mrefu kutafiti ubora na ukweli wa kikombe cha 'babu', na kushauri kwa nini wasiwaulize baadhi ya Wabunge na Mawaziri waliopo ndani ya bunge kama wamepona maradhi yaliyowafanya waende kupata kikombe kule Loliondo, Alisema Mh. Iddi Azzan Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, Dar es Salaam.

Kikombe cha 'Babu' ambacho hapo mwanzo kilikuwa kinaponya kwa neno la Yesu Kristo inaonekana neno hilo limepungua nguvu zake na kutufanya tuamini kuwa neno la Yesu Kristo limekuwa na tabia ya kuwa na nguvu ya soda. Tulitarajia kwa kumshirikisha Yesu Kristo katika tiba hii tusingetegemea mabadiliko kwa kuwa Yesu Kristo ni mtu mkweli. 'Babu' kama alitumia jina la Yesu Kristo kujipatia umaarufu ajue ya kwamba anamtia aibu kubwa Yesu Kristo hasa ukizingatia kuwa hakuna la maana lililopatikana Samunge zaidi ya kuongezeka kwa idadi ya makaburi. Dalili ya mvua ni mawingu na hii dalili mbaya kwa 'Babu' na kikombe chake tunashauri Serikali iendelee na mipango yake ya barabara na madaraja Samunge kwa ajili ya Wananchi wanaoishi huko kwani ni haki yao kupata huduma hiyo na si kwa ajili ya wateja wa babu 'Babu' kwani mwisho wake umekaribia na tulio wengi wetu tunaomba: "Ee Mola tuepushe na kikombe hiki"

JALSA SALANA 2012

Wanajumuiya wote wanaarifiwa kwamba, Jalsa Salana ya Kitaifa mwaka huu itafanyika kuanzia siku ya Ijumaa hadi Jumapili tarehe 28, 29 na 30 Septemba 2012, katika eneo la Jumuiya Kitonga Dar es Salaam. Inshaallah.

Wanajumuiya wote hasa wale wanaoishi jijini Dar es Salaam wanaombwa wajitahidi kuhudhuria Jalsa hiyo.

Ahmadiyya yang'arisha amani ya dunia Morogoro



Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood (katikati) akiongoza maombi mara baada ya upandishaji wa bendera kwenye mkutano wa mwaka wa mkoa wa Morogoro

Na DR. Pazi Kitabu
Mazongera-Morogoro

Ilikuwa siku ya tarehe mbili mwezi wa sita milango ya alasiri ambapo Jumuiya ya Waislam ya Waahmadiyya Tanzania chini ya uongozi wa Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh Tahir Mahmuud Choundry kwa mara nyingine tena iliwathibitishia Watanzania kuwa Jumuiya hii inafanya kwa matendo katika kuenzi amani duniani kwa kufanya Mkutano mkubwa wa amani Mkoani Morogoro kama ilivyoasisiwa na Kiongozi Mtukufu wa Jumuiya ya Ahmadiyya duniani Hadhrat Mirza Masroor Ahmad.

Mkutano huo wa amani ambao ulishuhudia viongozi wa dini mbalimbali wakitoa ushuhuda wa mafunzo ya dini zao namna yanavyofundisha na kusisitiza amani ambao ndio msingi mkuu wa dini ya tukufu ya Islam. Kwa kuwa tafsiri sahihi ya jina la Islam ni amani Mkutano huo ulikuwa ni fursa nzuri ya kuwaunganisha watu wa dini zote pamoja katika jina la amani, yaani Islam.

Mkutano huo ambao ulihudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mheshimiwa Joel Bendera ambaye alikuwa mgeni rasmi, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mheshimiwa Amir Nondo, Mstahiki Naib Meya wa Manispaa ya Morogoro Mheshimiwa Mary Lydia Joseph, diwani wa kata ya masika Mheshimiwa Tairo, mwakilishi toka ofisi ya kamanda wa polisi wa mkoa.

Viongozi wa dini za kikristo, hindu na masingasinga walikuwepo kuwakilisha dini zao katika mkutano huo wa amani ambao Mheshimwa Mkuu Wa Mkoa aliuita ni wa aina yake kuwahi kuhudhuria katika maisha yake ya kikazi.

Akitoa mada juu ya amani katika mkutano huo wa kihistoria, Muhubiri mashuhuri wa mihadhara ya dini ya Kiislam katika Mkoa wa Morogoro, Sheikh Bakri Abedi Kaluta alisisimua hadhara hiyo kwa kusema zaidi ya karne moja iliyopita, dunia ilishuhudia msukosuko mkubwa sana wa kutoweka kwa amani, uliosababishwa na baadhi ya viongozi wa dini waliotoa baadhi ya tafsiri potofu za maandiko matakatifu, na kusababisha watu wengi wamwage damu za watu wasio na hatia, wakidhani kuwa matendo yao hayo yatawafikisha moja kwa moja hadi Peponi, alisema katika utangulizi wa hotuba hiyo murua.

Sheikh alisema kuwa, karibuni watu wa dini zote mashuhuri walikuwa wakimsubiri nabii wao kudhihiri katika zama hizo ili kuja kuyarekebisha na kuyasuluhisha mambo ya kiroho na kimaadili yaliyokuwa yameparaganyika kupita kiasi katika kila pembe ya dunia.

Wahindu walikuwa wakisubiri ujio wa mtume wao, aliyejulikana kwa jina la Neha Kalank Avatar, aliyetabiriwa, ndani ya misahafu yao, kudhihiri mnamo zama zetu hizi hizi.

Wakristo nao walikuwa wakimsubiri Masihi wao Yesu Kristo, huku Waislamu wakiwa wakimsubiri Imam Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa. Wazoroaster nao wakawa wakimsubiri mtume wao aliyejulikana kwa jina la Mesio dar Bahme. Hata Nabii Budha, naye pia alitoa bishara ya kurejea tena duniani katika zama hizi hizi. Na hali kadhalika Guru Baba Nanak, naye pia alitoa bishara ya kuja kwa Guru Mkubwa katika zama hizi.

Aliendelea kusema kuwa, Guru Baba Nanaka aliyekuwa kiongozi mcha Mungu sana na aliyekuwa akipokea ufunuo toka kwa Mwenyezi Mungu aliwahi kusema:

"Utawala wa Wamughal utadumu kuanzia mwaka 1578 hadi 1897 wa himaya ya Bikram, halafu mtakatifu fulani atadhihiri."

Pia alisema: "Utafika wakati, katika siku za mwisho, ambapo watu wataacha kutenda sawa na maagizo ya misahafu yao, nao hawatafunga saumu wala kusali. Majogi, Masanyasi, Ma bharam Chavez na Mabrahmin watageuzwa kuwa ndio Maguru, yaani watakatifu. Hapo ndipo Mwalimu aliyekamilika atakapo waponda ponda wote. Hii ni Kudra ya kimbingu ambayo lazima itatekelezwa."

Pia akaongeza kwa kusema: "Mwalimu huyo aliyekamilika atakuwa ni Mwislamu, mcha Mungu na Mkweli na kwamba atatokea karibu na Batala, ndani ya wilaya ya Gurdaspur, akitokana na kabila la Wamughal.

Sifa zote hizi zimemuangukia Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya.

Hawa wote waliafikiana kuwa kiongozi mkubwa wa kiroho atadhihiri duniani mnamo siku zetu hizi za mwisho wa Dunia.



Sehemu ya wasikilizaji katika mkutano wa amani Morogoro - 2012

Alisema Sheikh Bakri katika hotuba yake iliyosheheni kila aina ya ushahidi.

Viongozi wa dini za kikristo, masingasinga na wahindu ambao kila mmoja alipata nafasi ya kueleza mafundisho na nasaha za dini zao kuhusu amani na kukiri kuwa amani ndiyo msingi mkuu wa kuwepo kwa dini zetu.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mh. Joel Bendera akiongea kwenye mkutano huu aliwataka Waislam kuwa mstari wa mbele kutoa maoni yao juu ya katiba na kuahidi kutoa katiba hizo kwa watu makundi mbalimbali ikiwemo Waislam ili waisome na kutoa maoni yao kwa uhuru na bila ya wasiwasi wowote.

Akizungumzia amani alisema amevutiwa mno na hotuba ya Sheikh Bakri na kueleza kuwa ametoa ufafanuzi mzuri unaovutiwa na yote aliyosema tumeyasikia na amabaye hajaelewa basi hilo ni tatizo lake na kuahidi kutoa ushirikiano kadri ya uwezo wake kwa Viongozi wa Jumuiya hii katika kuenzi amani hapa nchini.

Akisifia kazi nzuri inayofanywa Jumuiya ya Ahmadiyya hapa nchini katika huduma za Afya, Maji na Elimu, Alisema imekuwa ikifanya hivyo bila ya kujali dini, rangi, kabila wala itikadi ya mtu na kueleza kwa vitendo kauli mbiu ya Ahmadiyya inayosema "Mapenzi kwa wote chuki si kwa yeyote" alisema Mkuu wa Mkoa.

Mkutano huo wa amani ulihitimishwa kwa tafrija ya chakula kwa pamoja iliyofanyika katika viunga vya Jumuiya hapa hapa Kihonda.

Buriani Kanali Muammar Gaddafi lakini!!!

Pazi Kitabu Mazongera.

Siku ya tarehe 20 mwezi Oktoba mwaka 2011 Afrika ilimpoteza mwanamapinduzi shupavu kuwahi kutokea katika bara hili kwa miongo kadhaa na ni kifo kilichotokea ikiwa ni tofauti ya siku sita tu ambapo Watanzania tulikuwa tunakumbuka kifo cha Baba wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kilichotokea tarehe 14 mwezi Oktoba mwaka 1999. Huyu si mwingine bali ni Muammar Muhammad Abu Minyar al-Gaddafi au kwa jina maarufu ni Kanali Muammar Gaddafi.

Tofauti na kifo cha Mwalimu Nyerere ambaye alikufa kwa maradhi ya kansa ya damu, Kanali Gaddafi alikufa kifo cha kusikitisha mno kifo ambacho kila mtetezi wa haki za binadamu hatokiunga mkono kwa mazingira ya namna kilivyotokea. Alikuwa kwenye msafara wa magari kadhaa ambayo inasemwa labda alikuwa anaondoka kwenye mji



Kanali Muammar Gaddafi

aliozaliwa wa Sirte akashambuliwa na ndege za majeshi ya Ufaransa na kuua mamia ya walinzi wake na yeye kujeruhiwa kidogo lakini akalazimika kujificha kwenye mfereji mkubwa wa maji machafu katika mji huo. Majeshi ya wapinzani wake wakamkamata akiwa hana silaha yeyote wakaanza kumpiga makonde kumtukana na kumdhihaki na kumburuza bararani. Senad el-Sadik el-Ureybi askari wa jeshi pinzani wa Gaddafi amekiri kuhusika na kumkamata Gaddafi akiwa hai na alimpiga risasi ya kifuani, tumboni na kichwani na anasema ilimchukua takribani nusu saa kabla ya Gaddafi kukata roho. Inna lillahi wainna illahi raju'un. Zipo picha za video zinazoonyesha unyama huo na hutathubutu kuangalia mara mbili vitendo anavyofanyiwa mtu aliyewahi kuwa Kiongozi Mkuu wa nchi. Waziri mkuu wa Russia Bw. Vladimir Puttin ameviita kuwa ni vya kishenzi na kinyama na kamwe havikubaliki katika ulimwengu huu. Kwa hapa kwetu alisikika Waziri Mkuu Bwana Mizengo Kayanza Peter Pinda akisikitishwa na mauaji ya Kanali Gaddafi. Mh. Pinda alienda mbali zaidi kwa kusema, yaliyotokea Libya yanaweza pia kutokea hapa nchini. Kanali Gaddafi amekufa na msimamo wake usiyoyumba, kutetereka wala kutikisika. Amekufa na mawazo yake yasiyobadilika hata ikibidi kufa. Amekufa na imani yake dhidi ya wapinzani wake hata ikibidi kumburuza barabarani. Huyondiye Kanali Gadafi ninaediriki kumwita Simba wa Afrika aliyepata heshima



Gaddafi akiwa na Mh. Kikwete

ya kuogopewa na kuheshimiwa siyo tu na viongozi wa Afrika bali kwa sehemu kubwa ya dunia. Aliweza kuwaambia waziwazi mawazo yake hata maadui zake wakubwa wa nchi za Magharibi hali iliyopelekea wamuone kuwa ni kiongozi asiyefaa kwao. Gadafi hakupenda undumi la kuwili na hivyo hakuwa rafiki mzuri kwa viongozi wa nchi nyingi za kiarabu na ndio maana yeye alikuwa ni mwafrika zaidi kuliko uarabu.

Sisi kama Waislam wa Jumuiya ya Ahmadiyya kamwe hatushabikii mauaji ya kinyama ya namna ile si tu kwa Kanali Gaddafi bali kwa binadamu yeyote aliyeumbwa na Mwenyezi Mungu na akamuweka hapa duniani bila ya kujali dini, rangi, kabila au taifa lake. Tunaamini mauaji ya namna ile yana athari mbaya kwa jamii na kuleta taswira ya ulipizaji kisasi na kamwe hayo si mafundisho ya dini Tukufu ya Islam. Tunaendelea kuiombea Libya na dunia kwa ujumla kwa Mwenyezi Mungu ili mambo kama haya yaliyomkuta Kanali Gaddafi yasimkute binadamu mwingine yeyote. Amin.

Kanali Muammar Gaddafi aliingia

Endelea uk.7

Maudhui na fani katika
'Uongofu wa Tafsiri ya Qur'ani Tukufu

Na Mahmood Hamsin Mubiru - Dar es salaam.

Maudhui na Fani vikutanapo katika dhifa ya fasihi huwamba ki ajabu mithili kichwa na kofia, sahani na kawa, au chanda na pete. Na ni hivyo mzungupule Simba wa kwa Lumona Sheikh Kaluta Amri Abedi alivyokutanisha tena kwa umahiri mkubwa maudhui na fani katika utungo wake maarufu '***Uongofu wa Tafsiri ya Kurani Tukufu na husda ya Sheikh Abdallah Saleh Farsy***'.

Dhana hizi mbili Maudhui na Fani zina maana gani? Maudhui ni malengo, makusudio, dhamira ya msanii anayetaka kuwasilisha kwenye jamii ujumbe makhsusi. Ni risala na ujumbe maalumu ambao anaona unaweza kuleta mwanga palipo na giza, na matumaini kwa wale waliokata tamaa. Fani ni chombo kinachotumika na msanii ili kufikisha ujumbe wake. Fani isipokidhi mawazo, kazi hiyo haipendezi na inakuwa dabwa dabwa, mchuzi wake wa fani hiyo hauwi shata shata, na unakuwa majimaji kama mchuzi wa jogoo.

Maudhui na Fani vinatukumbusha kuwa mlo wa aina moja unakifu. Mlo unahitaji mabadiliko, kwani wa aina moja haumpi hamu wala balaghamu mlaji kusogelea mezani na chakula kuweka ndole. Wali kwa mathalani kuna biriani, pilao, wali wa maji, wali wa maua na wali wa mseto. Mabadiliko ni lazima kwa binadamu. Unaonaje bustani ingelikuwa na aina moja ya maua? Katu isingependeza. Mwandishi anatakiwa amnase msomaji, hivyo kwa kutumia kalamu Mwandishi anaweza kumfanya msomaji ahemee juu juu na asidiriki kukiweka chini kitabu hadi ukurasa wa mwisho.

Sheikh Kaluta Amri Abedi ni mahiri wa kufinyanga taswira kumna na kumliwaza msomaji. Kumburudisha, kumfanya atafakari, kumchekesha na kumuacha hana mbavu. Ni bingwa katika kuteua maneno na kuimba mahali kuimba kunapofaa. Ubingwa huu wa Sheikh Kaluta Amri Abedi uwekwa bayana katika kitbu alichoandika wakati yuko katika chuo kikuu cha Theolojia Rabwah Pakistani ya magharibi mwaka 1954. Ni jambo la kufurahisha kuwa wakati kinazaliwa chama cha TANU mwaka 1954 naye huko Pakistani Sheikh Kaluta Amri Abedi alikuwa anatayarisha silaha madhubuti ya kutukomboa kiroho.

Mwaka 1953 Sheikh Mubaraka Ahmad (HA), Mbashiri wa kwanza wa Ahmadiyya katika Afrika ya Mashariki alifasiri Kurani Tukufu katika Kiswahili. Jambo ambalo lilikuwa linaonekana haliwezekani. Masheikh wengi walipiga kelele, lakini Sheikh Mubaraka aliona hoja zao hazina mbele wala nyuma na hivyo kukamilisha kazi hiyo na kuiweka mbele ya wasomaji wa Kiswahili.

Watu wenye nia njema na mapenzi thabiti ya dini ya Islam walishangilia tafsiri hiyo na Mshairi maarufu Shaabani Robert akaiita tafsiri hiyo '***Mama wa Kiswahili***' na Mshairi mwingine maarufu wa Kiswahili -Saadan Abdul Kandoro alipata sururi na akaimba '***Isomwe iende mbele, Qurani Takatifu***'.

Sheikh Abdallah Saleh Farsy kwa upande wake alijawa na husda kwa kuona kuwa anatolewa tonge lake mdomoni

na kukumbushwa ya kuwa ingawaje yeye ni msomi, lakini 'avumaye baharini ni papa lakini wengine wapo'. Kutokana na hofu hiyo ya kukosa ulaji Sheikh Abdallah Saleh Farsy alishika kalamu na kushambulia tafsiri ya Kurani Tukufu iliyotolewa na Jumuiyya ya Ahmadiyya.

Katika kitabu chake alichokiita 'Upotofu wa Tafsiri ya Makadiani', ingawaje kijitabu hiki kilijaa uongo mwingi na porojo tele, Sheikh Mubaraka Ahmad (HA) aliona si busara kukiacha kijitabu hicho kupita hivi hivi bila kujibiwa. Ndipo Sheikh Mubaraka Ahmad (HA) akamtaka Sheikh Kaluta Amri Abedi aliyekuwa masomoni -chuo cha Wabashiri Rabwa Pakistani akijibu. Kazi hiyo aliifanya kwa nguvu zake zote na matokeo yake ni kazi hii nzuri iliyokidhi haja za kisomi Fani na Maudhui.

Maudhui ya kitabu hiki, tunaweza kuyagawa katika sehemu tatu; Je utume unaendelea? Je Nabii Isa (as) amekufa au atarudi duniani mara ya pili? Ukweli wa madai ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Ufafanuzi wa kina umetolewa juu ya mada hizo tatu na ushahidi mzito umesindikiza hoja hizo. Maneno ya ubabaishaji yasiyo kichwa wala miguu kama alivyofanya Sheikh Abdallah Saleh Farsy upuuzi huo haupatikani



Sheikh Kaluta Amri Abedi

katika kazi hii iliyofanywa kwa utulivu na kufuata kanuni ya 'Bila utafiti hauna haki ya kuzungumza'.

Hoja zimejengwa na zikajengeka na rejea zimetolewa kutoka katika Kurani Tukufu na Hadithi za Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Hapana shaka hadithi yoyote inayokwenda kinyume na Kurani Tukufu imewekwa pembeni, kwani hakuna ukweli nje ya Kurani Tukufu.

Sasa tuiingie katika kuchambua Fani alizozitumia Sheikh Kaluta Amri Abedi katika kufanikisha kazi yake hii ya sanaa.

I: Ushairi. Washairi wenzie akina Hamisi Amani Hamisi Nyamaume walikir ya kwamba Sheikh Amri alikuwa ni mshairi wa sifa. Walimheshimu na kumtegemea katika kuweka sawa mahali palipokwenda hovyo katika uwanja wa ushairi. Ni yeye aliyeitisha mkutano wa Washairi mwaka 1958 na pia amefanya kazi kubwa ya kuwafundisha watu sheria za utungaji wa mashahiri na katika Diwani nyingi ameandika utangulizi unaomsaidia msomaji aelewe vizuri sanaa hii ya ushairi. Hakuna alipotia fora kama katika utangulizi wa Diwani Waadhi wa Ushairi kilichotungwa na Mathias Mnyampala. Kwa sababu ya uzoefu wake katika bahari ya Ushairi ametumia vilivyo sanaa hii ili kufikisha ujumbe na kumpiga mweleka Sheikh Abdallah Saleh Farsy.

Baadhi ya beti ni fupi na nyingine ni ndefu sawa na haja. Uchaguzi wa maneno na mpangilio wa muwala ni vitu vinavyotusaidia kuelewa vizuri jambo linalosemwa. shairi la kwanza katika kitabu hicho ni shairi la vita, lisemalo:

1.Tu katika jeshi, la Muhammadi,
kwenye kitali.
Na Amiri jeshi, ndiye Mahadi,
shujaa kweli.
Ujapo uzushi, na ukaidi,
twaukatili.

Na kila utashi, wa mahasidi,
utadhalali.
Kiwingu cha moshi, kiwafisidi,
kwa yao zuli.

2. Ndimi asikari, wa Asikari,
Wake Jalali.
Sikhofu jeuri, khasa jeuri,
za udhalali.
Wajapo jasiri, kina ayari,
kwa ufedhuli.
Hushika hodari, yangu khanjari,
penye kitali.
Nikawakhasiri, kwa hoja nzuri,
zenye akili.

3. Nihudhuriapo, kwenye medani,
zenye kitali.
Hugandama papo, hadi mwishoni,
kama jabali.
Ndipo nishindapo, kwa kila fani,
za kusaili.
Haki ing'aapo, nani shetani,
wa kukabili?
Ndipo wajutapo, kina fulani,
kwa idhilali.

Lakini vita ya kalamu. Vita ya kutetea dini tukufu ya Islam. Vita ya kuweka bayana taadhima ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Jeshi hili ni mali ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw), lakini jeshi lazima liwe na Amiri Jeshi. Na mshairi wetu anatupa jina la Amiri jeshi huyo ni nani - "Na Amir jeshi ndiye Mahadi", yaani Seyidna Ahmad (as). Amiri jeshi huyu si wa mchezo mchezo ni "Shujaa kweli". Na jeshi hili analoliongoza kila panapotokea uzushi na ukaidi vyote vinateketezwa. Na wote wanaozusha mambo na kuleta husda hawa wote wanafunikwa kwa kiwingu cha moshi wasiweze kupumua. Katika jeshi hilo la Muhammad (saw) linaloongozwa na Masihi Seyidna Ahmad (as) yumo askari ambaye ni muandishi. Askari huyu ni jeuri hasa jeuri wa idhilali. Na wanapotokea Maayari hapo huongeza mapambano, mapambano ya hoja zinazoingia akilini. Akiingia vitani hatoki mpaka ushindi umepatikana.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

TANZIA

Mzee Jafari Ali Nyamkwasu Kirungi afariki dunia.

Na Ismaili I. Mkoggas - Dar es salaam

Mnamo tarehe 30/06/2012 kwa masikitiko makubwa tumepokea habari za kifo cha aliyekuwa Mzee wetu mpendwa - Jafari Ali Nyamkwasu Kirungi kilichotokea huko Mkongo Rufiji mkoani Pwani.

Mzee Jafari ni miongoni mwa wazee wakongwe walioipokea Jumuiyya mnamo miaka ya 50 huko Rusende Rufiji. Mzee Jafari alianza kujisikia vibaya juu ya hali yake mnamo siku ya tarehe 29/06/2012 majira ya jioni akiwa amekwenda sokoni kujitafutia mahitaji yake ya nyumbani. Ndipo aliporudishwa nyumbani kwa usafiri wa pikipiki, na baada ya hapo hali yake ilizidi kuwa mbaya kadri muda ulivyozidi kwenda. Usiku kucha hata ilipofika asubuhi ya tarehe 30/06/2012 saa mbili asubuhi Mzee alitutupa mkono Innalillahi wa Inna ilaihi rajiuun.

Hivyo Mzee Jafari amekuwa ni Mzee wa mwisho katika mtaa wa Singida waliokuwa wakiendelea kuishi hapo huko Mkongo Rufiji, kuiga dunia, kwani kabla yake kuna wazee waliomtangulia kutoka mtaa huo ambao kwa Mkongo ulijulikana kama Singida mtaa wa Makadiani. Wazee hao waliokuwa ni pamoja na wafuatao:- Mzee Msongoro Magenge, Mzee Rajabu Muhenga Mkoggas, Mzee Ali Nyamkwasu, Mzee Sultani Mwera, Mzee Ramadhani Ngirini, Mzee Athumani Mtindasi Kisoma, Mzee Shabani Malinda, Mzee Makomea Mwera, Mzee Abdallah Mchawi, Mzee Mbwana Kingwande, Mzee Ibrahim Mkoggas na Mzee Mbwana Mchawi. Hawa ni wazee waliojipanga katika mtaa huo wa Singida ulipo Msikiti wa Jamaat.

Wazee wengine waliishi katika mitaa mingine kijijini hapo. Inshallah historia zaidi ya Mzee wetu huyu basi itatolewa katika toleo lingine.

Bustani ya Washairi

SWALI ‘ALAA NABIYYIINA

1. Ewe Mpweke Wahidi, Mola wetu Subhana
Umetukuka Wadudi, kwako tudhaifu sana
Umetuthamini sana, kumuumba Muhammad
Umetutukuza sana, umati wa Muhammad
Swali ‘alaa nabiyyiina, Swali ‘alaa Muhammad
Swali ‘alaa Rasulina, Swali ‘alaa Muhammad

2. Ya Ilahi Ya Swamadi, jicho lisiyekuona
Unao wako muradi, sisi Nawe kujuana
Umijeweka bayana, kupitia Muhammad
Apendaye kukuona, swiratwi ni Muhammad
Swali ‘alaa nabiyyiina, Swali ‘alaa Muhammad
Swali ‘alaa Rahimiina, Swali ‘alaa Muhammad

3. Kwenye haya makusudi, Umetuma waungwana
Wamo akina Daudi, Issa Mussa na Haruna
Katika hao mabwana, mkuu ni Muhammad
Wa mwanzo na akhiriina, mbora ni Muhammad
Swali ‘alaa nabiyyiina, Swali ‘alaa Muhammad
Swali ‘alaa Sayyidina, Swali ‘alaa Muhammad

4. Ndiye bwana wa zuhudi, dunia aloikana
Mwalimu wa Tawhidi, mfano wake hakuna
Kwa ufundi wa kusana, khatamu ni Muhammad
Mleta athari sana, muhuri ni Muhammad
Swali ‘alaa nabiyyiina, Swali ‘alaa Muhammad
Swali ‘alaa Habibiina, Swali ‘alaa Muhammad

5. Umemjaza suudi, baraka kila namna
Kugusa yake jasadi, kipofu hupana ona
Vyote tunavyoviona, kaumbiwa Muhammad
Mwanga wa huu mchana, ni nuru ya Muhammad
Swali ‘alaa nabiyyiina, Swali ‘alaa Muhammad
Swali ‘alaa Raufina, Swali ‘alaa Muhammad

6. Umemtuma anadi, kutuita kila kona
Ukampa ustadi, wa wagonjwa kutupona
Katika zote hazina, neema ni Muhammad
Katika vyenye maana, thamani ni Muhammad
Swali ‘alaa nabiyyiina, Swali ‘alaa Muhammad
Swali ‘alaa Kariminaa, Swali ‘alaa Muhammad

7. Dunia yote baridi, nyoyo zimegandamana
Pekee ndiye faridi, wafu wafufuke tena
Anayetaka kupona, shafii ni Muhammad
Anayependa kunona, tajiri ni Muhammad
Swali ‘alaa nabiyyiina, Swali ‘alaa Muhammad
Swali ‘alaa Shafi’ina, Swali ‘alaa Muhammad

8. Ndiye mlea junudi, maula wa maulana
Kukaa naye baidi, ni kujidhulumu sana
Katika zote safina, nahodha ni Muhammad
Zama hizi za fitina, mwokozi ni Muhammad
Swali ‘alaa nabiyyiina, Swali ‘alaa Muhammad
Swali ‘alaa Maulaana, Swali ‘alaa Muhammad

9. Imetufikia Idi, waja tupate pendana
Kwa sifa ya Ahmadi, imara tumeshikana
Sisi naye kuungana, sababu ni Muhammad
Kwa pamoja tunanena, mpendwa ni Muhammad
Swali ‘alaa nabiyyiina, Swali ‘alaa Muhammad
Sali ‘alaa Rafiiqina, Swali alaa Muhammad

10. Ametufunza jihadi, tuwe ni wapole sana
Tuupinge ufisadi, bila fimbo kuchapana
Kuepuka kugombana, amani ni Muhammad
Jamiul ‘alamiina, Rehema ni Muhammad
Swali ‘alaa nabiyyiina, Swali ‘alaa Muhammad
Swali ‘alaa Imaamanaa, Swali alaa Muhammad

Abdulrahman M. Ame

MAISHA SASA YALIVYO

1 Ah! hali inatisha, siyo ya kuhadithiwa
Wengi inatuendesha, na sivyo ilivyokuwa
Inatishia maisha, baraka imepunguwa
Sasa tumeelemewa, kwa mzigo wa maisha

2 Si mchezo yanatisha, yaogofya kuzaliwa
Shida zinatuendesha, dhiki tumezichukuwa
Taabu tumejitwisha, hatuoni pa kutua
Sasa tumeelemewa, kwa mzigo wa maisha

3 Kila mmoja na kasha, matatizo kagawiwa
Kila tukijaribisha, japo kujitutumuwa
Ugumu huuzidisha, pasiwe la kutatuwa
Sasa tumeelemewa, kwa mzigo wa maisha

4 Chakula cha kujilisha, kupika na kupakuwa
Hatukimudu cha Isha, cha mchana majaliwa
Penginepo tunakesha, bila tonge kuambuwa
Sasa tumeelemewa, kwa mzigo wa maisha

5 Mchele bei komesha, imeparara ingawa
Kuupata kwetu kesha, vigumu wali kuliwa
Kwa sima twajibukisha, tena kwa kujikamuwa
Sasa tumeelemewa, kwa mzigo wa maisha

6 Unga hawakuushusha, bei tumeongezewa
Kitoweo ni rabsha, nyama, samaki ikawa
Na mkaa wa kuwasha, bei ghali twanunuwa
Sasa tumeelemewa, kwa mzigo wa maisha

7 Maharagwe tunarushwa, jinsi tunavyouziwa
Na nazi imepaishwa, ni kama ya kukuniwa
Kila upande twatishwa, hatuna hata afuwa
Sasa tumeelemewa, kwa mzigo wa maisha

8 Mafuta taa na kisha, dizeli wanonunua
Petroli mezidisha, na nauli imekuwa
Mambo si mazuri hasha, sisi wa kunusuriwa
Sasa tumeelemewa, kwa mzigo wa maisha

9 Kabla kukhitimisha, kodi ya nyumba mekuwa
Nayo wameziboresha, sasa tumeongezewa
Kodi wameizidisha, hoehae tumelewa
Sasa tumeelemewa, kwa mzigo wa maisha

10 Basi ninatamatisha, tulo duni tu wakiwa
Tumekwama kimaisha, ya Allah unaliliwa
Hali yetu rekebisha, uiweke sawasawa
Sasa tumeelemewa, kwa mzigo wa maisha

Al-Ustadhi Khamisi S.S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala rangi tatu
S.L.P 376 Dar es salaam

SHEMEJI KULA

1 Shemeji Bin Ng’ambage, tungoni umelalama
Walia kuna mazonge, watu wanakusakama
Ndoa yako kuna genge, linaitia nakama
Ndoayo si ya lawama, shemeji kula limbwata

2 Hukuoa bintiyo, si kweli wanavyosema
Washikao rai hiyo, ni majuha maamuma
Au wamejaa choyo, kuona unajinoma
Ndoayo si ya lawama, shemeji kula limbwata

3 Binti hawi mwanao, kwa kumtendea wema
Lazima awe mzao, kwa damu kukuandama
Ndipo itakuwa mwao, kumuoa ni lawama
Ndoayo si ya lawama, shemeji kula limbwata

4 Asiye shangazi yako, na usiyemwita mama
Si zao la mke wako, si ulul - arkama
Hana kizuizi kwako, kumuoa si dhuluma
Ndoayo si ya lawama, shemeji kula limbwata

5 Wala hukufanya tusi, vipi wakupe shutuma?
Waonao ni nukusi, mila zinawasukuma
Kwetu hazina nafasi, zamani tumezikama
Ndoayo si ya lawama, shemeji kula limbwata

6 Ndoayo haina tenge, kisuna iko salama
Mkeo usimtenge, kwa kuhofu uhasama
Wa hao wenye mawenge, dini waloweka nyuma
Ndoayo si ya lawama, shemeji kula limbwata

7 Hao ni waivu kwako, wenye chuki na husuma
Wana nyingi chokochoko, uchaji umewahama
Kuna giza wapitako, si njia mustakima
Ndoayo si ya lawama, shemeji kula limbwata

8 Kungwi nakupa hongera, heshima na taadhima
Umefanya jambo bora, mbele ya Mola Karima
Bali umetia fora, kwa kufanya suna njema
Ndoayo si ya lawama, shemeji kula limbwata

9 Kuoa umjuaye, amehimiza Hashima
Na aige atakaye, huo ni mfano mwema
Kwa hili achukiaye, imaniye si timama
Ndoayo si ya lawama, shemeji kula limbwata

10 Mke wako ishi naye, kwa idhini ya Rahima
Tena upendane naye, kwa pendo lenye adhama
Ni halali zaa naye, mpate kizazi chema
Ndoayo si ya lawama, shemeji kula limbwata

Abdullah Hamisi Mbanga (Kungwi) -
Dar es salaam

TUMBO

1 Machungu haya maisha, kila siku ni msoto
Kwa mawazo yasoisha, nalia kama mtoto
Shibe inayolitosha, ni mchanga na kokoto
Vichwa vinawaka moto, tumbo watuhangaisha

2 Tumbo unatukondesha, hofu hofu tumbo joto
Usiku kucha twakesha, tukiwaza michakato
Hadi twahisi presha, kwa kupata mchecheto
Vichwa vinawaka moto, tumbo watuhangaisha

3 Ugomvi usioisha, tumbo halijali pato
Hata ndani kikiisha, tumbo halina mpito
Fahariye kulilisha, hapo ngoma kitokito
Vichwa vinawaka moto, tumbo watuhangaisha

4 Ukweli nawakumbusha, mambo ya tumbo mazito
Haramu wahalalisha, kusudi upate vito
Haki ukaipindisha, ukinge njaa mpwito
Vichwa vinawaka moto, tumbo watuhangaisha

5 Na dunia imekwisha, imepoteza mvuto
Akili zetu zawasha, kugombania mapato
Ya kuume twakomesha, twaenda mbio kushoto
Vichwa vinawaka moto, tumbo watuhangaisha

6 Tumbo lasahaulisha, nyumba ulifunga fito
Lo! Leo waidondosha, upite njia mkato
Safari kuifupisha, uchakate mchanyato
Vichwa vinawaka moto, tumbo watuhangaisha

7 Mwisho ninakhitimisha, ogopa siku ya wito
Tumbo litatukwamisha, litutie mkong’oto
Ewe mwenye kuwezesha, tulinde na mkamato
Vichwa vinawaka moto, tumbo watuhangaisha

Mwl. Najat Fakim Said, Mafisa, Kilindi - Tanga.

SITARA NI VAZI JEMA

1 Ewe Rabi Rahmani, niongoze kwa yakini
Niandike ya mizani, ninenayo ya manani
Pia ziguse nyoyoni, ndugu zangu waumini
Sitara ni vazi jema, vaa utaheshimika

2 Salam kwa wana mama, mazuri nawaambia
Nisimamapo kusema, ni uwezo wa jalia
Na pia ninayo sema, ni vema kuzingatia
Sitara ni vazi jema, vaa utaheshimika

3 Sitara tumeziacha, twaiga mambo si mema
Ya Mwenyezi tumeacha, ndugu zangu wanamama
Na kwambia ndugu macha, tushindaneni kwa wema
Sitara ni vazi jema, vaa utaheshimika

4 Kuzibana zetu nguo, si vema hiyo tabia
Unaleta tamanio, na zambi kujipatia
Hasa we muaminio, ndugu umesha sikia
Sitara ni vazi jema, vaa utaheshimika

5 Shungi ukijifunika, jambo zuri lenye shani
Wanawake wa sitara, huheshimiwa njiani
Washonao za sitara, zina shuka hadi chini
stara ni vazi jema, vaa utaheshimika

6 Na majivuno si mema, Mola wetu katwambia
Na tushindane kwa wema, Kuruani yatwambia
Na elimu kufuzama, ya dini na ya dunia
Sitara ni vazi jema, vaa utaheshimika

7 Dunia tambara bovu, ina muda huchanika
Acha kutenda uovu, kuvaa nguo za kaka
Waja jishika mashavu, siku hiyo ikifika
Sitara ni vazi jema, vaa utaheshimika

8 Tuachane na dunia, hebu turudi kwa Mola
Omba maombi sawia, nusura anayo Mola
Ipe mgongo dunia, Aokoae ni Mola
Sitara ni vazi jema, vaa utaheshimika

9 Nywele bandia kuweka, amekataza Rasua
Wangapi waliziweka, na sasa wamejifia
Utakuja nikumbuka, haya ninayokwambia
Sitara ni vazi jema, vaa utaheshimika

10 Tamaa kuachilia, ndugu zangu nawambia
Mauti yanasogea, omba kwa kunyenyekea
Baya ni baya tambua, na ina mwisho dunia
Sitara ni vazi jema, vaa utaheshimika

11 Sitara kwanza kwa mama, mtoto pia afata
Ayasema Maulana, dunia hii ni tata
Na mkumbuke karima, duniani tunapita
Sitara ni vazi jema, vaa utaheshimika

12 Wassalaam ninatoa, ni mwisho wa kutamka
Kalam ninaachia, na kitini nainuka
Vizuri kuzingatia, upate zako baraka
Sitara ni vazi jema, vaa utaheshimika

Mariam O. Kilimo, S.L.P 605 - Ifakara Mjini

Endelea uk.7

Bustani ya Washairi

Kutoka uk. 6

KIFO CHA MAJID SUDI

1. Ai! Msimbe nalia, kifo cha Majidi Sudi,
Mwenzetu katangulia, ameitwa na Wadudi,
Ende Peponi tulia, penye kivuli baridi,
Kifo cha Majidi Sudi, pengo kwa Ahamdiyya.

2. Mwalimu Sudi hakika, mlezi wa maabadi,
Tutazidi mkumbuka, kwa dua zetu zaidi,
Majidi ameondoka, kamwe tena hatorudi,
Kifo cha Majidi Sudi, pengo kwa Ahamadiyya.

3. Kufa kwetu kawaida,viumbe ili muradi,
Unapofikia muda, hayupo wa kukaidi,
Kifo hakina msada, wala hakina miadi,
Kifo cha Majidi Sudi, pengo kwa Ahamadiyya.

4. Nitamuenzi daima, kwa alioniahidi,
Kwamba nisiache soma, ya Masihi Ahmadi,
Kwenda kusali lazima, nikisikia mnadi,
Kifo cha Majidi Sudi, pengo kwa Ahamadiyya.

5. Ahamadiyya kamili, humkosi Masijidi,
Muhimu kwake kusali, Mungu akimuhimidi,
Na michango mbali mbali, atoapo kwa juhudi,
Kifo cha Majidi Sudi, pengo kwa Ahamadiyya.

6. Kanambia Kamdula, hiyo ndio itikadi,
Yote ni juu ya Mola, kwa hilo kuwa sitadi,
Mataifa na kabila, Uisilamu ni jadi,
Kifo cha Majidi Sudi, pengo kwa Ahamadiyya.

7. Kadhalika ushairi, niuwekee samadi,
Usitawike vizuri, nimsifu Muhammadi,
Kwa dhima na ikirari, nimsifie Mahadi,
Kifo cha Majidi Sudi, pengo kwa Ahamadiyya.

8. Huo usia pekee, kaniachia Majidi,
Na mimi niupokee, niweze kuwa mweledi,
Gazetini nitokee, kama ndege Hudihudi,
Kifo cha Majidi Sudi, pengo kwa Ahamadiyya.

9. Tamati ya beti tisa, nisizidishe madadi,
Kama ningefika Jalsa, vile ilivyonibidi,
Tungeonana kabisa, kitonga kwenye muridi,
Bwana Beta ni shahidi, mambo mengi nimekosa.

Professor: Kamdulla Msimbe,
Ahmadiyya Muslim Jamaat, S. L. Posta, 1 Morogoro.

Buriani Kanali Muammar Gaddafi lakini!!!

Kutoka uk. 4

madarakani katika mapinduzi yaliyofanyika mwaka 1969 na kuiongoza nchi hiyo kwa miaka 42 na hivyo kuwa kiongozi wa pekee kutawala kwa muda mrefu katika miaka hii ya 1900.

Alizaliwa mahali paitwapo Qasr Abu Hadi nje kidogo katika mji wa Sirte na alikulia katika mahema yaliyopo Bedouin katika jangwa lililopo pembeni mwa mji huo wa Sirte. Anatoka kwenye kabila dogo liitwalo Qadhadhfa. Babu yake Kanali Gaddafi aitwaye , Abdessalam Bouminyar aliwahi kupambana hadi kufa dhidi ya watawala wa Italy na kuonekana kuwa amekufa kishujaa mnamo mwaka 1911.

Kanali Muammat Gaddafi alikuwa na mapenzi makubwa na Rais wa Misri aliyepindua mwaka 1952 Bw. Gamal Abdel Nasser. Alikuwa na cheo cha Meja Jenerali lakini alisema ataendelea kutumia cheo cha Kanali na alivaa sare za cheo cha Kanali kwa maisha yake yote.

Kanali Muammar Gaddafi alikuwa ni kiongozi kipenzi kwa wananchi wake na Afrika nzima. Alikuwa ni mtu wa mfano wa kuigwa miongoni mwa Viongozi wa kisiasa katika ulimwengu huu wa sasa kwani alifanikiwa kuifanya Libya ambayo ardhi yote ni jangwa kuwa ni mahala salama kiustawi wa maisha na mahitaji ya binadamu. Elimu, afya, makazi na mahitaji mengi ya kijamii yalipatikana bure katika uongozi wa Kanali Gaddafi. Aidha alikuwa ni mfadhili wa mataifa mengi ya Afrika na hasa yale ya wanyonge kifedha, Kanali Gaddafi alikuwa ni msemaji wao na katu hakuwaogopa wakubwa wa Ulaya Magharibi na Marekani kwa dhuluma zao na ndio maana mbele ya macho yao Kanali Gaddafi alionekana kuwa kama si gaidi basi anafadhili ugaidi kwani kwao wao ukipingana nao tu inatosha kuwa gaidi.

Tumuombee kwa Mwenyezi Mungu kama kuna kosa amelifanya amsamehe na Allah anatosha kuwa mlinzi wake huko akhera.

Sisi kama Jumuiya ya Ahmadiyya tunacho cha kusema kuhusu Kanali Gaddafi na inawezekana kifo chake kimekuja kipindi hiki ili kiwe somo kwa watawala mbalimbali wa sasa wanaofanya dhihaka



Gaddafi akiwa na Gamal Abdel Nasser



Zulfikar Bhutto

na mzaha juu ya Ahmadiyya. Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya hii ya Ahmadiyya aliwahi kupata ufunuo unaosema kuwa "Mimi nitamlinda kila atakaekusaidia" na "Mimi nitamfedhesha kila atakaekufehedhesha".



Dr. Iddi Amini Dada

Mnamo mwaka 1974 viongozi watano waliojiita ni wa kutoka nchi za Kiislam walikutana mjini Lahore nchini Pakistan. Nao ni King Faisal Abdullah wa Saudi Arabia, Rais Zulfikar Bhutto wa Pakistan, Rais Iddi Amin Dada wa Uganda, Rais Anwar Saadat wa Misri na Kanali Muammar Gaddaf wa Libya. Pamoja na mambo mengine waliyojadili katika maendeleo ya dini ya Kiislam kubwa waliazimia kuutangazia ulimwengu kuwa wafuasi wa Jumuiya ya Ahmadiyya si Waislam na hivyo hawana haki ya kujitangaza kuwa ni Waislam na popote duniani wasichukuliwe kuwa ni Waislam. Hilo lilikuwa ni azimio ambalo walikubaliana kama viongozi wa nchi kuunda sheria dhalimu za kutowatambua na kuwanyima haki zinazomhusu Muislam hapa duniani. Na ujumbe huo ulifika sehemu kubwa ya dunia na mabaraza mbalimbali ya dini ya kiislamu duniani waliuchukua ujumbe huo kuwa rasmi na ni halali na ndio unaofanyiwa kazi hadi hii leo. Hivyo ukiona mtu yeyote anakuambia kuwa Ahmadiyya si Muislam ni mawazo yaliyotokana na maazimio ya kikao hicho.

Kwa bahati mbaya au ni mpango wa Mwenyezi Mungu Marais wale wote walipoteza nafasi zao za Urais aidha kwa kuuawa au kwa kudhalilika muda mfupi baada ya kikao kile isipokuwa Kanali Muammar Gaddafi. Tunaamini aliachwa hai hadi sasa kwa sababu maalum.

Rais Zulfikar Bhutto wa Pakistan ambaye alikuwa msomi wa sheria kutoka Chuo Kikuu cha mjini California nchini Marekani na Chuo Kikuu cha Oxford cha nchini Uingereza. Alipata mafanikio makubwa ya kiutendaji kama Rais kwa kuwa alizungukwa na wataalamu mbalimbali ambao baadhi yao walikuwa ni Waahmadiyya. Ndiye muasisi wa mipango na uwezo wa kinyuklia wa sasa nchi hiyo, Aliyekuwa mshauri na msaidizi wake mkuu katika mpango wa nyuklia ni Profesa Abdul Salaam aliyekuwa pia ni Ahmadiyya mahiri. Rais Bhutto ameshiriki kwa kiasi kikubwa baada ya kikao kile kuidhalilisha Ahmadiyya nchini mwake kwa kuweka sheria dhalimu mara tu baada ya kikao kile cha mwaka 1974. Alipinduliwa na Bw. Zia ul Haq na pamoja na kutetewa na Mataifa mengi duniani alinyongwa mnamo tarehe 4 April 1979.

Rais mwingine aliyeshiriki kwenye kituko hicho ni Muhammad Anwar al-Saddat wa Misri ambaye alikuwa ni mshiriki mkubwa katika kupiga marufuku Ahmadiyya nchini mwake.

Aliuawa katika shambulio baya kabisa la kigaidi kuwahi kutokea katika mauaji ya Rais mjini Cairo tarehe 6 Octoba 1981. Shambulio hilo lililaaniwa na watu mbalimbali duniani ambalo pia alijeruhiwa Bw Hosni Mubarak ambaye alikuja kuwa Rais wa nchi hiyo.

King Faisal bin Abdul-Aziz Al Saud ambaye alikuwa ni mwenyeji wa mkutano ule mbaya kabisa na ndiye aliyekuwa mfadhili mkubwa wa mataifa mengi ya kiarabu kwa wakati ule alitumia fedha zake katika kuhakikisha Ahmadiyya aipigi hatua katika ulimwengu huu kwa kufadhili makundi mbalimbali ya harakati dhidi ya Jumuiya ya Ahmadiyya duniani.

Ndiye aliyekuwa pia mfadhili mkubwa wa kila Rais wa nchi atakaekuwa tayari kupinga Ahmadiyya ili ipotee katika ramani ya dunia. Ni mwaka mmoja tu toka



King Faisal bin Abdul-Aziz Al Saud

kikao kile kifanyike King Faisal Bin Abdul Aziz Al Saud aliuawa na mtoto wa kaka yake tarehe 25 mwezi Machi 1975 aitwaye Faisal bin Mussaid. Alimpiga risasi wakati wakisalimiana kwa kumkumbatia kijana huyo ambaye alikuwa ametoka nchini Marekani. Na hapo ukawa mwisho wa maisha ya King Faisal Bin Abdul Aziz Al Saud ambaye alizaliwa mwaka 1906.

Rais Field Marshal, Alhaji, Dr. Iddi Amini Dada wa Uganda aliyezaliwa tarehe 1 Januari 1923. Alikuwa na wake watano wanaotambulika nao ni Maryam Amin, Kayi Amin, Nora Amin, Madina Amin na Sara Amin na alikuwa na watoto wapatao arobaini. Katika kutekeleza maazimio ya kikao cha mwaka 1974 aliendeleza kufanya maamuzi magumu dhidi ya Ahmadiyya. Kwanza alipiga marufuku Tafsiri ya Qur'an Tukufu iliyo katika lugha ya Luganda kazi iliyofanywa na Jumuiya ya Ahmadiyya miezi kadhaa baada ya kutoka kwenye Kikao kile. Na aliendeleza mpango wake wa kuwafukuza watu wote wenye asili ya bara la Asia wapatao 80,000. Kwa kuwa Waahmadiyya wengi ni watu wa bara la Asia aliamini atakuwa amedhoofisha silsila ya Ahmadiyya nchini mwake. Kwa ushauri wa Muammara Gaddafi aliweza kutaifisha mali za watu hao na wengi walikimbia nchi hiyo. Iddi Amin Dada alikuwa kiongozi mwenye maadui wengi



Muhammad Anwar al-Saddat

hapa duniani kwani alipewa majina mabaya akiwa bado ni kiongozi wa nchi. Majina kama dikteta, fashisti na hapa Tanzania alijulikana kama nduli. Hizi ni sifa ambazo zinaonyesha hakuwa kiongozi anayependwa na haiba yake iliendelea kupungua na kujikuta anajiingiza katika vita na Tanzania bila ya kuwa na sababu zenye mashiko. Na kama Iddi Amin Dada angejua, ile haikuwa vita ya kupigana lakini ilikuwa lazima apigane ili aondoke madarakani. Tarehe 11 April 1979 Mji Mkuu wa Kampala ulitekwa na majeshi ya Tanzania, askari wa Muammar Gaddafi walitekwa na yeye akakimbia kwa helikopta hadi nchini Libya alikoishi hadi mwaka 1980. Baadaye akahamia kwenye nchi rafiki ya Saud Arabia ambako afya yake ilikuwa dhaifu kwa maisha yake yote hadi alipofariki tarehe 16 Agost 2003 kwa kile kinachoelezwa na madaktari kuwa ni multiple organ failure yaani viungo vya mwili kushindwa kufanya kazi. Alipoteza Urais na akafa akiwa mtu dhalili kwa kusaidiwa na Serikali ya Saud Arabia na Kanali Muammar Gaddaf.



Gaddafi akiwa na Putin

Wakati tunaendelea kupinga mauaji ya Marais wote hao walioshiriki kufanya maamuzi dhalimu dhidi ya Ahmadiyya kwa kuwa ni jukumu letu kama Waislam kuhakikisha dunia inakuwa mahala salama kwa binadamu kuishi hatuwezi kupinga ukweli wa kile walichokifanya viongozi hawa na kile kilichowakuta na matokeo ya dhuluma waliyofanya dhidi ya Islam. Wako Waahmadiyya mamia kwa mamia waliouawa na wapo wanaoteswa kwa sababu ya maamuzi ya viongozi hawa. Ukiangalia mikanda ya video ya mauaji wanaofanyiwa Waahmadiyya nchini Indonesia, Pakistani na hata Bangladesh inazidi ile ya Kanali Muammar Gaddafi. Waahmadiyya mbalimbali wanateswa kwa kuburuzwa wakiwa hai hadi kufa, wako wanaopigwa risasi hadi kufa, wako wanaopigwa mawe hadi kufa kwa sababu tu wanasema "hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah na Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu", wanasema Ahmadiyya hana haki ya kutoa kalima kwa sababu si muislam. Huo ulikuwa ni uamuzi mmbaya kuwahi kufanywa na Viongozi wa kisiasa hapa duniani. Kanali Muammar Gaddafi ambaye aliwaita wapinzani wake kuwa paka, panya na sisimizi alikamatwa kwenye mfereji wa maji machafu uliojaa paka, panya na sisimizi katika mji wa Sirte. Tumehifadhiwa Kanali Muammar Gaddafi aje kuwa somo sisi wa kizazi kipya na ni kazi yetu kupitia historia.

Toka uamuzi wa mwaka 1974, Jamaat Ahmadiyya imepata maendeleo makubwa zaidi ya mara 100, matarajio yao hayakutimia na Islam chini ya bendera ya Ahmadiyya imekuwa ikifanya kazi nzuri kueneza dini. Jamaat Ahmadiyya imeingia takribani katika nyingi za kiarabu na imekuwa ikishika kasi na kutangaza ya ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa kupitia matangazo ya MTA kwa kiarabu.

Viongozi wa kisiasa waliopo na wakaokuja baadaye hili linatosha kuwa somo kubwa juu ya mitazamo yao kwa Ahmadiyya. Tunaendelea kumuomba Mwenyezi Mungu yaliyotokea Libya, yasitokee siyo tu Tanzania bali na kwingine duniani. Inawezekana historia inapotoshwa juu ya kifo cha Gaddafi lakini ukweli utabaki pale pale. Buriani Kanali Muammar Gaddafi lakini "Mimi nitamfedhesha kila atakaekufehedhesha".

"Mwelewe Maulvi Nuruddin"

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. na kutafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Jamil Rahman Rafiq

Kutoka toleo lililopita

MAWAIDHA YA MWISHO

Dkt. Bhagwan Das Kushta, Mwalimu Mkuu wa shule moja katika Saharanpur, alihudhuria mbele ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. tarehe 22 Machi 1913, na akatangaza kukubali Islam. Akamsihi Mwislamu mpya huyo akisema:

"Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mungu pekee Aumbaye na kumjaalia mtu mahitaji yake yote. Hakuna yeyote mwingine anayestahiki kuabudiwa wala kuchukuliwa kuwa Mungu. Kumwabudu yeyote minghairi yake ama kumsujudia ni ushirikina. Pamoja na kuagiza kuamini Umoja wa Mungu, Islam inataka pia kumwamini Muhammad s.a.w. kuwa mtumishi Wake na Mjumbe Wake. Kwani, katika zama zilizopita alipodhihiri duniani wakati wowote mtu mwema, wafuasi wake, baada ya muda fulani, wakamfanya mungu. Hiyo ndiyo ilitendeka kumhusu Ram Chandra a.s. na Krishan a.s. Yesu a.s. pia akafanywa Mungu, akaitwa Mwana wa Mungu, ingawaje alisema: Mbona waniita mwema? Hakuna mwema isipokuwa Mungu. Kwa hiyo, Mtume Mtukufu s.a.w. akaogopa isije yeye naye akafanywa mungu akaongeza katika shahada: 'Hakuna mwabudiwa ila Mungu,' na kwamba yeye yu mtumishi na Mjumbe wa Mungu.

Jiha ya pili ya Islam ni huruma kwa viumbe wa Mungu. Zaka na Hija hutilia moyoni huruma ya watu, na sala na saumu humfanya mtu kujihurumia, kuna baraka kubwa katika saumu. Hiyo humzoesha mtu kuepukana na matumizi yasiyo halali ya kitu chochote; kwani yule anayejitenga mbali na kile kilicho halali katika saumu, lazima atatenganana kilichoharamishwa na Muhammad s.a.w. kama akimwamini yeye. Basi maana ya kanuni ya imani ndiyo kusisitiza Umoja wa Mungu na kwamba Muhammad s.a.w. ni mtumishi Wake na Mjumbe Wake, na kwamba sala, saumu, Haji na zaka vimewekwa kwa faida ya mtu binafsi na pia kwa jamii nzima. Kuna faida gani kumnyunyuzia mtu maji kama alama ya kukubali imani? Yesu alisema, ni rahisi ngamia kupita ndani ya kitundu cha sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu."

Katika kharifu (msimu baina ya kiangazi na kipupwe) na kipupwe cha mwaka 1912-1913, Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a. alikwenda kutembelea Misri na Hijaz na katika safari hiyo akahiji pia. Akarejea Qadian Februari 3, 1913. Mnamo kiangazi cha mwaka huo akaamua, kwa kupata kibali cha Hadhrat Khalifatul Masihi r.a., kuanzisha kutoa gazeti la kila wiki ambalo Hadhrat Khalifatul Masihi akaliita *Al-Fadhl*. Tolea la kwanza lilitolewa Juni 19, 1913. Baadaye likawa gazeti la kila siku na sasa tangu zaidi ya nusu karne ni gazeti la Jumuiya ya Ahmadiyya.

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akashikwa na homa kali sana mnamo Juni 25. Keshoye, ijapokuwa alikuwa bado dhaifu, akatoa darasa la Qur'an Tukufu, na mwishowe akanena:

"Niuguapo, nachelea kwamba pengine ndio mwisho, safari hii pia nikafikiri hivyo. Nikasali *Rakaa* mbili. Katika *Rakaa* ya kwanza baada ya sura *Fatiha* nikasoma sura *Dhuha* (93) na katika *Rakaa* ya pili Sura *Inshirah* (94). Kisha nikashughulikia kumsifu Mungu na kuomba ghofira. Ndipo nikaomba dua ambayo nina yakini imepokelewa. Narudia ili nyote mshirikiane katika hii. Nayo ndiyo hii: Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mungu, Mjuzi wa kila kitu, Mpaji. Hamna mwabudiwa minghairi ya Mungu, Mola wa Arshi kuu. Hamna mwabudiwa ila Mungu, Mola wa mbingu na ardhi, Mola wa Arshi Tukufu. Nakuomba njia za kuvutia rehema Yako, na njia imara za kupata msamaha Wako, na hadhi kubwa ya kila wema, na usalama katika kila dhambi. Usiache kosa langu lolote bila kulisamehe, wala ghamu yangu yoyote bila kuiondoa, wala mahitaji yangu yoyote ya kweli bila kuyatimiza, Ewe Uliye Mrehemevu sana. Mola, tumeelemewa sana kutoka kila upande, Islam imeshambuliwa vikali. Waislamu ni walegevu, wana elimu haba ya dini, au ya Qur'an Tukufu, au ya mfano wa Mtume Mtukufu s.a.w. Maadui wanasonga mbele. Mola, mwinue mtu mwenye kuvutia, asiye mzembe, shujaa sana, mvumilivu, mwenye kukimbilia daima kuomba dua, mwenye kutimiza matakwa yako, mtaalamu wa ujuzi wa Qur'an Tukufu na Hadithi za kweli. Tena Umjaalie Jumuiya ambayo wanajumuiya wake wawe na sifa hizo zote. Mola, kama kuna majaribio, basi wajaalie imara, na Usiwatwishe mizigo wasiyoweza kuibeba (2:287); na Uwakuze jinsi nilivyoomba.

Nahisi Mungu Atatimiza utashi wangu. Nyinyi nanyi mwombe kwa moyo huo, na muwe wasaidizi katika njia ya Mungu."

Keshoye ilikuwa Ijumaa, akawasihi jamii ya waabuduo katika hotuba ya pili kama ifuatavyo:

"Sina la kukazania isipokuwa maombi. Dumuni kufanya maombi. Nawasisitizieni hiyo kwa manufaa yenu. Sitaki kutoka kwenu chochote, hata kwamba mwinuke kwa kuniheshimu. Kama ningalitazamia chochote kwenu, ningalifanya kosa kubwa kabisa la utovu wa shukurani kwa Mungu. Je, Yule Mungu Aliyenijaalia fadhili zake sikuzote, zaidi kuliko nilivyotazamia, Atanifanya sasa niwategemeeni katika uzee wangu kwa siku zangu chache zilizobakia?

…. Fadhili zake zifululizazo zanilazimisha niwe Wake kikamilifu. Nguvu zangu zote ni fadhili Zake, heshima zote na taadhima nilizo nazo ni zawadi Zake."



Maulana Hadhrat Hakeem Nuruddin Khalifatul Masih I r.a.

Ni la kushangaza kwamba mawaidha yote ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a ya kusisitiza mwafaka na umoja baina ya wanajumuiya, maonyo yake yote kuhusu matokeo ya kuogofya ya mafarakano na fitina, yakawaathiri wafitini wagumu kwa kitambo kidogo tu, kama yaliathiri kwa vyoyote. Kwa hakika wakaonekana kukaza ukaidi wao. Ni kweli ya kwamba jumuiya kwa jumla kwa kutahadharishwa ipasavyo na kuonywa ikasalimika katika ujanja mbaya wa watu wachache wenye mikono mirefu wasiotaka kupatana; na huo kweli ulikuwa ufaulu mkubwa. Hata hivyo ni jambo la kujutia kwamba mtengano haukuweza kuepukika.

Uongozi wa wafitini ulikuwa na nguvu katika Lahore. Afya ya Khalifatul Masihi r.a. ilipoendelea kwa vyovyote kuwa hafifu na ikaanza kuharibika, kundi la wafitini likaanza kufanya propaganda kwa ushupavu kukabili hatari isiyoepukika. Hatua ya kwanza waliyochukua ni kwamba wakaanza kutoa gazeti kutoka Lahore waliloita *Paighame Sulh* (Ujumbe wa Amani). Toleo la kwanza lilitolewa Julai 10, 1913. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akawa mnunuzi wake, lakini baadaye akakataa kulipokea, kwa kuona madhara ya sera zake na kazi yake hata kwamba akaliita *Paighame Jang* (Ujumbe wa Vita). Mara kwa mara ahadi za uaminifu kwa Khalifatul Masihi r.a. zilichapishwa, lakini walipungukiwa nia. Ilipigwa kampeni mfululizo kumvunjia heshima Shaibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a. Walichelea isije Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad, japo alikuwa kijana tu, akachaguliwa kuwa *Khalifa* baada ya Khalifatul Masihi r.a. ambaye hakuficha kwamba alimheshimu sana Sahibzada. Itikadi na mafundisho ya Jumuiya ya kupambanua yaliyotolewa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. yalielezwa mara kwa mara na Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. na hadi wakati huo yalikuwa yanakubaliwa na viongozi wa wafitini wenyewe, yakaanza kubomolewa taratibu na kuzimuliwa na wafitini kwa nia ya kupendwa na Waislamu wengi wasiokuwa Waahmadiyya.

Ijapokuwa afya yake iliendelea kuharibika Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alitoa darasa la Qur'an Tukufu nzima katika mwezi wa Ramadhani mnamo Agosti – Septeba 1913.

Shambulio kubwa zaidi lilifanywa kwa niaba ya wafitini kutoka nyuma ya pazia nyembamba na ya woga katika Oktoba 1913, kwa sura ya vijitabu vidogo viwili bila ya jina la mwandishi, kimoja baada ya kingine katika kitambo kifupi, vilivyoitwa *Idh-harul Haq I* na *Idh-harul Haq II* (kudhihirisha haki). Vilikuwa vichafu na vya aibu, vilivyojaa madai ya uwongo ya uchongelezi dhidi ya Hadhrat Khalifatul Masihi na watu wa familia ya Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s., akiwemo Hadhrat Ummul Muminin r.a. pia. Kweli hii kwamba vilitolewa hivyo kwa kushauriwa na viongozi wa wafitini – ingawa walikana – inahakikishwa na maneno ya Mahriri wa *Paighame Sulha* la 16 Novemba 1913, ambayo ni haya:

"Tumeona katika vijitabu hivyo kwamba maneno mengi yaliyoandikwa humo hayana shaka hata kidogo kwamba ni ya kweli.... Kama *Ansarullah* ya Lahore ikiona inafaa kujiingiza katika habari hii na kukusudia kuandika chochote dhidi yetu ili kuzalisha kuelewana kubaya kwa sababu tumeyaunga mkono maneno yaliyomo ndani ya vijitabu hivyo, hapo lawama itakuwa juu yao kama tukichapisha lolote kwa kujibu."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaiagiza *Anjuman Ansarullah* kutayarisha na kuchapisha majibu ya vijitabu hivyo. Muswada wa majibu ulipopelekwa kwake, akaukagua na akandika juu yake: *Paigham (Sulha)* linastahili kupata lawama elfu kwa kutuletea ujumbe wa vita kwa kuchapisha barua yake wazi, na kwa njia hiyo limetangaza unafiki wake. Amelaaniwa yule anayezindua msiba ulalao.

Majibu yalitolewa katika vijitabu viwili: *Khilafat Ahmadiyya* kikachapishwa Novemba 23, na *Idh-ahare Hakikat* tarehe 28 Novemba 1913. Majibu hayo yakathibitika kuwa yenye kuathiri mno kama kanusho kamili la masingizio na uchochezi ya kuadhiri na ya uwongo yaliyoandikwa katika vijitabu vya kuchukiza, na yakailinda Jumuiya kikamilifu dhidi ya fitina ambayo vijitabu vyao vilikusudia kuchochea.

Khalifatul Masihi r.a. alipougua sana baada ya kuanguka kutoka juu ya farasi jike, akaona katika ruya kwamba mtu fulani ametia rupia moja mfukoni mwake. Akaagua kwamba atapata mwana. Ruya hiyo ikatimia tarehe 18 Novemba 1913 ambapo alijaaliwa mwana wa tano aliyemwita Abdullah.

Mkutano wa Mwaka wa 1913 ulifanyika Desemba 25-27. Wahudhuriao walikuwa wengi zaidi kuliko mwaka uliopita. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akiendelea kuhutubia alinena:

"Kutimiza mapatano ni jambo la faradhi. Nawaelekezeni kwenye ahadi mojawapo ili muweze kutafakarikwambamnaitekeleza. Ndiyo ahadi ya utii mliyofanya nami. Tena kati yenu kuna wenye hali mbaya wasemao: *Khalifa*, ati, ni nini? Yu mkongwe. Angalieni, sikilizeni na kumbukeni ya kwamba Mungu Mtukufu Amenifanya *Khalifa*, nami simtegemei yeyote kati yenu kwa chochote. Nimekwisha omba dua kulindwa na matokeo ya uzee, na Yeye Amenihifadhi. Amenijaalia ujuzi wa Neno lake. Kunilaumu kwenu hakukubaliwi na Mungu. Yeye Ana ghera kwangu. Tubuni kwa fikira yenu mbovu. Yeye Amehifadhi kikamilifu nguvu zangu. Sifa zote njema ni Zake kwa fadhili Zake zote.

Nyinyi hamna uhuru wa kueneza habari zinazohusikana na ulinzi au hatari. Mwapaswa kumfikishia chochote cha aina hiyo Amiri au Mwenyekiti wenu ili aweze kuchukua hatua yoyote ifaayo. Waliochapisha vijitabu viwili, *Idh-harul Haq*, na barua moja ya wazi kwa *Ansarullahi*, na kuendeleza majadiliano juu ya *Ukhalifa*, hawakuwa na madaraka kufanya hivyo. Barua ya wazi iliniudhi sana moyo wangu. Tena mtu fulani akaniletea kadi iliyochapishwa na akaniomba ruhusa kuichapisha. Nikamwambia hiyo ni kinyume cha Qur'an. Akaomba ruhusa ya kufanya jambo alilokwisha fanya tayari. Watu kama hao wanavunja maagizo ya Qur'an, na wanatafuta kufarakisha watu ambao Mungu kwa rehema yake Ameunganisha kwa mkono wa mtu mmoja. Mjihadhari kwao. Tena mtu fulani alisema kwamba nilipoanguka kutoka juu ya farasi jike, hiyo ikamaanisha kuwa nimeanguka kutoka *Ukhalifa*, na kwamba hiyo ilikuwa kwa sababu ya ukosefu wa uimara. Huku ni kuelewa vibaya sana kashfi moja ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. Mungu Ameniagiza kuhusu majibu ya hayo yote. Tenganeni na watu kama hao na epukaneni na fikara mbovu"

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Safari ya Sadr Khuddam katika mikoa ya kanda ya kati na kanda ya magharibi

Na Mwandishi wetu -
Dar es salaam

Tarehe 20/05/2012 saa moja asubuhi ndani ya msikiti wa Jumuiyya ya Ahmadiyya Masjid Salaam Mnazi Mmoja, Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry -Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiyya ya Ahmadiyya aliongoza maombi ya kimya kwa ajili ya kuomba rehema, huruma, ulinzi na msaada wa Mwenyezi Mungu uwe juu ya wanaosafiri.

Safari itakayochukua siku takriban kumi yenye umbali wa kilometa 1442. Hii ni safari ya Sadr Khuddamul Ahmadiyya na wajumbe wawili kutoka Majlis ya Khuddam Taifa kutembelea wanatanzim katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma. Dhumuni likiwa ni kukutana na wanajumuiyya hususan Khuddam na Atfal kwa ajili ya kufahamiana, kuangalia utekelezwaji wa shughuli za wanatanzim katika matawi yao, na kupeana mipango mipya na namna ya utekelezaji.

Katika msafara huo Sadr Khuddam Bw. Ally Hamisi Mbambwa alifuatana na Muhtamim Tabligh Bw. Salum Ibrahim Ndatama, Muhtamim Atfal Bw. Mudathir Zaidi na Dereva Bw. Ismail Ibrahim Mkoggas.
Safari ilianza rasmi, na kituo cha kwanza kilikuwa Chalinze kwa ombi maalum kutoka kwa Muhtamim Tahrik-e-Jadid Bw. Fadhili Mikila kuwa msafara upate kifungua kinywa hapo. Alhamdulillah. Haikuwa chai tu, bali ni zaidi ya chai. Pia msafara ulisimama Morogoro Masjid Nusrat na Dodoma Masjid Baitul Hameed. Hatimae msafara uliingia Manyoni majira ya saa mbili usiku. Mwalimuwa Jumuiyya Khalifa Jailani pamoja na Khuddam na Atfal waliupokea msafara na kuukirimu hasa sawa na mafundisho ya Islam.

Tarehe 21/05/2012 saa kumi (10) Alfajri, msafara uliondoka Manyoni na kuelekea Mkoa wa Tabora kupitia njia ya mkato ya Itigi. Kwa fadhila za Allah msafara uliingia Tabora mjini majira ya saa tano asubuhi. Sawa na ratiba ya Sadr siku hiyo kulikuwa na vikao viwili. Kimoja Tabora Mjini na kingine katika Jamaat ya Kilungu. Hivyo saa sita kamili msafara uliondoka Tabora mjini kuelekea Kilungu Jamaat.

Sauti za Ahlan wasahlan wamarhaba zilisikika katika eneo lililozungukwa na miti yenye vivuli mwanana, ziliashiria kuwa tumewasili hasa katika Jamaat ya Kilungu. Jamaat imara, maarufu, kongwe na yenye wanajumuiyya makini, imara weledi wa mambo, wakarimu na wenye imani hasa ya dini yao. Khuddam, Atfal na Ansarullah walimkaribisha Sadr na ujumbe wake kwa mapenzi ya hali ya juu kwa kukumbatiana kulikutanguliwa na Assalaam Alaikum. Pembeni yao walisimama Lajna Imaillah na Nasrat wakionesha nyuso za furaha na shukurani kwa Allah kwa ujio huo kufika salama.

Baada ya sal aya Adhuhuri na Alasiri kikao kilianza rasmi. Sawa na taratibu za Jumuiyya na Islam kwa ujumla, kikao kilianza kwa usomaji wa Kurani Tukufu iliyosomwa na Mwalimu Ally Ahmad, shairi lilisomwa na Bw. Yahya Mgeleka kisha yakafuatia maombi ya kimya na kiapo cha Tanzim kwa Khuddam na Atfal. Baada ya kiapo ulifuatia utambulisho kwa pande zote mbili, kwa wageni na wenyeji.

Baada ya utambulisho huo, ilifuatia risala ya Qaid Khuddam Bw. Adam Mgeleka kwa Sadr Khuddam. Katika risala yake Qaid alianza kwa kusema, sifa zote njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu na Rehema na Amani zimfikie Mtume Muhammad (saw). Alisema, tawi la Kilungu ni tawi mama ambalo lina matawi yaliyochini yake matano (5) nayo ni Milumba, Migungumalo, Mwakashindye, Ipungu na Ibambo. Khuddam katika tawi la Kilungu ni 18 na Atfal 22. Akielezea shughuli za Tanzim katika tawi alisema wanatanzim wanaendelea na shughuli mbalimbali za kijamaat kama vile Tabligh, Waqar Amal na Tarbiyyat. Pia alisema zipo changamoto kadhaa zinazowakabili katika matawi yao. Changamoto hizo ni pamoja na kukosa Msikiti kama vile Jamaat Migungumalo, Ipungu, Ibambo pamoja na Milumba. Hata hivyo katika Jamaat ya Milumba, Khuddam wameendelea kufanya kazi za kujitolea takriban kwa miaka mitatu (3) juu ya ujenzi wa Msikiti na hivi sasa wamefikia hatua ya linta.

Akijibu risala ya Qaid, Sadr sahib kwanza alimshukuru Mwenyezi Mungu na pia alitoa shukurani kwa Majlis Khuddam kwa ushiriki wao katika shughuli za Jamaat pia aliwakumbusha wanatanzim kuwa Jumuiyya ni mali yao. Hivyo ni wajibu wao kutoa kipaumbele katika kutatua matatizo yanayoikabili Jamaat. Akitoa mfano kwa wanatanzim wa tawi la Milumba ambao wamejitolea kujenga msikiti kwa nguvu, wakati na mali zao, alisema huo ndio mfano bora ambao unapaswa kuigwa kwa zile Jamaat ambazo haizna misikiti. Na pale watakapokwama watakuwa na haki sasa ya kuomba Makao Makuu iwasaidie ili wakamilishe mradi wao.



Sadr Khuddamul Ahmadiyya (wa mwisho nyuma kulia) pamoja na msafara wake akiwa kwenye picha ya pamoja na wanajamaat wa tawi la Nguruka mkoani Kigoma

Baada ya kujibu risala ya Tanzim Sadr alisema katika ziara yake ya kutembelea matawi, anayo mambo kadhaa atakayo yawasilisha kwa wanatanzim.

(i) Maandalizi ya Ijtimaa ya Tanzim ya Khuddamul Ahmadiyya. Sadr alisema tarehe 15, 16 na 17 mwezi Juni 2012 itafanyika Ijtimaa ya kitaifa huko Dar es salaam katika eneo la Jamaat huko Kitonga. Sadr alisema Ijtimaa ni kikao ambacho kila Khuddam na Atfal anawajibika kuhudhuria. Hivyo ni wajibu kwa kila mmoja kufanya maandalizi kuhakikisha anahudhuria kikao hicho. Akiendelea kufafanua Sadr alisema katika Ijtimaa yatakuwepo mashindano mbalimbali ya kimwili na kiakili. Ni wajibu wa Qaid wa tawi na Majlis Amila yake kuwahamasisha na kuandaa mikakati kwa Khuddam wahudhurie na kushiriki mashindano hayo.

(ii) Mchango wa Ijtimaa. Sadr alisema ni wajibu kwa kila mwanatanzim kuchangia mchango wa Ijtimaa. Kila Khuddam anawajibika kuchangia sh.5,000 na Atfal sh.3,000 mara moja kwa mwaka. Mchango huo unapaswa kulipwa ndani ya mwaka wa kitanzim ambao huanza tarehe 01 Novemba na kumalizika tarehe 31 Octoba ya mwaka unaofuata. Sadr alisema ni wajibu sasa kwa kila mwanatanzim kuhakikisha analipa mchango huo kabla ya tarehe 31 Octoba ya mwaka huu. Na si lazima mtu atoe kwa mkupuo bali hata kidogo kidogo ilimuradi mchango ukamilike ndani ya wakati.

(iii) Kikao cha shura. Kikao cha shura ni kikao cha kutathmini shughuli zinazofanywa au kutekelezwa na Tanzim kwa mwaka uliopo na kuandaa maazimio ya shughuli mbalimbali zitakazotekelezwa mwaka unaofuata. Mipango hiyo ni pamoja na kujadili bajeti ya mapato na matumizi ya mwaka uliopo na ujao. Kikao hicho kina wajumbe maalum ambao wanatakiwa kushiriki. Qaid wa tawi ni mjumbe wa shura kikatiba. Pamoja nae kila tawi lenye Khuddam kuanzia 1 - 20 atachaguliwa mjumbe mmoja. Tawi pamoja na kupata wajumbe wawili pia tawi linayo haki ya kuandaa na kutuma agenda zitakazojadiliwa katika shura hiyo.

(iv) Utumaji wa taarifa za kila mwezi Makao Makuu. Taarifa ni jambo la muhimu sana kati ya tawi na Makao Makuu. Hivyo kila Qaid ahakikishe anafanya kikao cha kila mwezi na Majlis Amila yake ili kukusanya taarifa za utekelezwaji na mwezi husika na kupanga mipango ya mwezi unaofuata kisha taarifa zitumwe Makao Makuu kwa Sadr Majlis. Katika utumaji wa taarifa Sadr aliwakumbusha utekelezaji wa shughuli zilizo orodheshwa katika Kalenda ya Tanzim. Pia Sadr alitoa barua kama mfano watakao utumia kupeleka maombi ya kufanya aidha Waqar Amall (kazi za kujitolea) au Khidmat Khalq (Huduma kwa viumbe) katika Ofisi za serikali.

(v) Mpango maalum kwa Atfal wote nchini. Katika mpango huu, Sadr alimtaka Katibu wa Atfal Bw. Mudathir Zaid kutolea maelezo. Akitoa ufafanuzi juu ya mpango huo, Muhtamim Atfal alisema; Atfalul Ahmadiyya ndio Khuddam wa kesho. Kwa kujua umuhimu wa Khuddam katika Jamaat, ni wajibu mkubwa kuwaandaa Atfal tulionao sasa ili waje kuwa Khuddam bora na muhimili wa Jamaat. Kwa kuliona hilo, Majlis Khuddamul Ahmadiyya Taifa imeandaa mpango maalum kwa Atfal wote nchini kuwa, wanatakiwa kuhudhuria Miskitini siku ya Ijumaa kwa ajili ya sala. Na baada ya sala watawajibika kubaki kwa ajili ya kupata mafunzo mbalimbali. Watalala hapo na siku ya Jumamosi baada ya sala ya Alasiri ndipo watarejea majumbani kwao. Tanzim ya Khuddam ndio itakayosimamia zoezi hili kwa kufikisha maombi kwa Mashehe, Walimu na Wanajumuiyya wenye elimu ya dini kutoa mafunzo hayo sawa na vipindi watakavyoviandaa. Aidha kuhusiana na gharama za uendeshaji hususan chakula, Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry alishatuidhinisha kuwa wazazi wa watoto na wanajumuiyya kwa ujumla watoe mchango wa fedha au chakula kwa ajili ya darasa la watoto (ni muhimu kuzingatia kuwa fedha hizi hazikatiwi risiti). Huu ni mchango kuhakikisha darsa linakuwa endelevu bila ya kukwazo chochote. Hivyo Muhtamim Atfal aliwaomba Wabashiri, Wazazi na Wanajumuiyya wote kuhakikisha Atfal wanafika Msikitini na Darasa linaendelea. Pia aliwaeleza kuwa ripoti kuhusu maendeleo ya Madarasa hayo zitumwe Makao Makuu.

Baada ya maelezo hayo Sadr sahib alitoa ruhusa ya kuuliza maswali pamoja na kutoa maoni. Kisha Sadr alitoa katiba ya Tanzim ambapo alimtaka kila mwanatanzim ahakikishe anaisoma na kuelewa ili ajue wajibu wake na utaratibu wa Tanzim kwa ujumla. Mwisho kikao kilifungwa kwa maombi yaliyoongozwa na Sadr majira ya saa 10 alasiri.

Baada ya kikao kulikuwa na dhifa maalum kwa wageni na wenyeji. Mara tu baada ya chakula ujumbe wa Sadr uliwaaga wenyeji na kurudi Tabora Mjini kwa ajili ya kikao cha huko.

Masjidil -Fadhil ni moja ya misikiti maarufu katika nchi yetu ambao unamilikiwa na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. Msikiti huu uko pembezoni mwa kituo kikongwe cha mabasi cha Tabora Mjini. Huu ni msikiti wa kwanza wa Jumuiyya ya Ahmadiyya nchini uliojengwa na wafungwa wa Kiitaliano 1944. Pamoja na kupitisha miaka mingi, bado hadi leo msikiti huu unameremeta kwa uzuri wa ajabu. Ndani ya Msikiti huu ndipo kilifanyika kikao cha pili cha Sadr Khuddam na ujumbe wake.

Kikao kilianza mara baada ya sala. Qaid wa tawi Bw. Shabani S. Matongo alitoa risala fupi kabla ya kumpatia Sadr uwanja wa kuwafikishia aliyowaletea. Katika risala yake Qaid alisema, tawi la Tabora Mjini ni tawi kongwe au tuseme ndio tawi mama la matawi yote nchini. Lakini pamoja na hayo wao katika Tanzim ya Khuddam bado wanachechemea. Hivyo wanatoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa ujio kutoka Makao Makuu ambao anaamini huenda ukawapa uhai mpya.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Falsafa ya safari ya Mbali - Miiraj

Kutoka uk. 12

haupimiki. Hakika hayupo anayestahili kusifiwa kwa sifa njema isipokuwa Mwenyezi Mungu tu, Mola wa viumbe vyote. Huumba Apendavyo. Apendalo hufanyika bila ngenga. Anaposema kun mara huwa.

Baada ya hapo, Tumwa Bashiri akaoneshwa mto Kauthara. Naam, wakaufuata hadi ulipokomea. Wakafika kwenye nyumba njema yenye neema tele. Wakaona viumbe ambao Mtume (saw) hajawaona hata siku moja. Si hivyo tu, bali hata masikio yake hayajasikia wala khabari zao kusemwa wala mawazo hayajapata kuwaza. Viumbe hao walionwa wapo mlangoni wamesimama. Loo! Ni kweli, sadaka moja utowayo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu utalipwa mara kumi. Anayetaka karadha, hutaka kwa matatizo yake. Mtume (saw) akaiona pepo. Pepo hiyo imepambwa kwa dhahabu, marijani na zumaridi. Imenakishiwa kwa zambarujudi na yakuti yenye rangi ya kuvutia. Ni sehemu ya mapumziko hasa.

Jibril na Mtume (saw) wakaoneshwa Jahanamu, kule kwenye moto mkali. Huko wakaona vituko vya adhabu, naye Nabiyullah (saw) hakuweza kustahamili kutazama. Akatokwa na fahamu ikazulu akili yake. Seyidna Jibril akamtuliza na wakati huo huo akarejewa na fahamu zake kama kawaida.

Mtume Muhammad (saw) baada ya hapo, akaingia daraja la Nne kwa sababu Seyidna Jibril alikuwa mwepesi. Hata hivyo Mtukufu Mtume Muhammad (saw) akasema kwamba pale ndipo kikomo chake wala hawezi kamwe kusogea mbele zaidi ijapo shubiri moja. Basi pakaja kiwingu cha rehema kikamfunika Mtume (saw) kisha akaulizwa ana haja gani ambayo anataka Mwenyezi Mungu Aelezwe. Jibril akamtuliza Mtume Muhammad (saw) na kumuuliza; "Una haja gani ewe mpenzi, haja ambayo unataka nikamweleze Mwenyezi Mungu" Mtume (saw) akanena "Haja yangu niitakayo hasa ni kuwa hiyo siku ya siku mimi niwe Kinga ya umati wangu. Ninyooshe mabawa yangu ili wafuasi wangu usiwaguse ule moto wa Jahanmu".

Naam, Mtume Muhammad (saw) mara akaingia katika hijabu naye akazipita hizo zote. Hapa, Mtukufu Seyidna Muhammad (saw) akamuona Mwenyezi Mungu kwa mboni ya macho yake mawili. Mtume Muhammad (saw) akaanza kutoa salaam Atahiyyatu yake Jalali. Mola Akamjibu Muhammad (saw) "Na Salaam iwe kwako, ewe Mtume mteule. Wewe ni mtu wa kuwekwa mahala pema". Mtukufu Mtume (saw) alipomuona Mwenyezi Mungu Ana kwa Ana, hakuweza kuinuwa kinywa chake kutamka chochote. Alikumbwa na bumbuwazi. Mwenyezi Mungu Akamwambia Muhammad! "Omba utakalo utapewa" Mtume Muhammad (saw) akaporomoka na akaenda sijida kumhimidi Allah. Akaomba Muhammad; "Ee Mola wangu, mja wako Seyidna Ibrahimu ni mpenzi wako. Je, na mimi nina sehemu gani?" Allah Akamjibu na kumwambia Muhammad; "Nawe pia u-kipenzi changu vile vile, hilo ulielewe. Daudi tumempa Zaburi na Suleimani alimiliki majini na ndege. Bali wewe ndiwe awali wa Mitume na ndiwe wa akheri. Mimi nitajwapo jina lako nawe litatamkwa nyuma. Kama vile Isa alikuwa anaponya vilema na wenye ukoma, nawe halikadhalika utafanya hivyo, bali zaidi. Wewe Nimekupa Arshi isiyokwisha. Umati wako ndiyo bora kuliko nyimati nyingine yoyote. Siku ya kiyama utakuja kuona makafiri kama watakana hayo, basi waache. Utambue kwamba wewe ndiwe muombezi wa siku hiyo, siku iliyo nzito kweli kweli.

"Sasa nakuambia haya Nikupayo hakuna yeyote aliyepewa. Kwa hiyo nihimidi na unishukuru. Nakufadhisha swala khamsini. Haya chukua wewe mwenyewe pamwe na umati wako itabidi mziswali kila siku".

Baada ya maelezo hayo, hijabu ya nuru ikaondoka naye Seyidna Muhammad (saw) akarejea pale alipokuwa Jibril. Wote wawili wakafuatana kurejea hiyo safari. Wakati wanarejea wakakutana na Nabii Musa. Seyidna Muhammad (saw) akampasha khabari zote za huko atokako. Nabii Musa akamwambia Seyidna Muhammad (saw) kwamba umati wake hawawezi kuswali swala hamsini kwa siku. "Nakushauri urejee kwa Allah umwombe tahfifu ya kwamba akupunguzie kwa sababu watu wako dhaifu mno". Baada ya kupata ushauri huo kutoka kwa Nabii Musa (as) Mtume (saw) akarejea kwa Mwenyezi Mungu kuwaombea tahfifu watu wake. Na Mwenyezi Mungu Akamkubalia. Akapunguziwa, kutoka khamsini hadi swala tano. Seyidna Muhammad (saw) alipofika kwa Nabii Musa kwa mara nyingine, akaambiwa arejee tena kwa Allah, kwa sababu hata hiyo swala tano itakuwa ngumu kwa watu wake ikawa kwenda na kurudi. Lakini mwisho akasadifu swala tano kamili.

Basi, Subhana wata'ala Alimwambia Mjumbe wake Muhammad (saw) kwamba mtu yeyote atakaye swali swala tano kwa nyakati zake na kwa ukamilifu, malipo ya kila swala malipo yake ni ya swala kumi. Hapo tena Mwenyezi Mungu hatabadili kauli yake. Mwenye kunuia kutenda amali njema, Allah humpa fadhila. Na yule anayetenda wema wenyewe, basi Mwenyezi Mungu Anamlipa malipo mema. Wema mmoja, malipo mara kumi kamili. Na yule anayenuwia kutenda mabaya, lakini asitende, huyo ataandikiwa sawa na njia yake. Yule atakayetenda ataandikiwa dhambi moja kwa moja.

Baada ya hapo, Seyidna Jibril na Seyidna Muhammad (saw) wakateremka hadi uwingu wa chini. Wakaona vumbi na moshi vimetanda. Wakasikia sauti ya kelele. Mtume (saw) akamuuliza Jibril hao wali watu gani. Akaambiwa hao ni mashaitwani wamezuiwa kuona mbingu. Usiku huo huo, Jibril na Muhammad (saw) wakashuka Baitul-Mukadasi, kwenye ile nyumba takatifu tangu zamani. Hapo, wakamuona yule Buraku bado yu pale pale walipomuacha awali akiwasubiri. Ndiyo baada ya kutamka Bismillahi, Mtukufu Mtume (saw) na Seyidna Jibril wakampanda Buraku. Wakii bado wakienda, njiani wakaona ngamia wengi ambao walikuwa wanatokea Shamu. Makureishi walipomuona Buraku, walikimbia hadi kustajabisha



Baadhi ya watu wamechora picha ya Buraq kuwa mnyama mzuri, kitu ambacho ni cha kubuni.

mmoja wao pale alipoanguka na kuvunjika mguu wake asiweze kuinuka. Jibril na Mtume (saw) walifika Makka usiku wa manane bado hakujacha. Mtume (saw) aliwaza sana kichwani kwake. Alikuwa anakhofia Makureishi namna watakavyokadhibisha khabari za safari yake ya mbinguni pindi atakapowaeleza. Akingali bado Mtume (saw) akiwaza, kufikiri na kutafakari, mara akamuona mabuuni Abujjahal. Abujjahali akamdadisi na kumdhihaki Mtume (saw), "Nakuona ewe Muhammad uso wako ni wenye huzuni nyingi, je una jambo gani kubwa mno lililosababisha hata sura yako isikunjuke? Naomba unieleze ili nami nielewe, maana ninavyokuelewa leo haupo katika ile hali tuionayo kila siku". Mtume (saw) akasema, naam, nitakuambia yale yanayonipa wasiwasi kiyasi hiki. "Ni kwamba usiku wa leo nilisafiri safari ya mbali sana. Nimefika mbinguni na nimemuona Mwenyezi Mungu, Mola Jalali. Amenipa mambo mazito kwa ajili ya ummati wangu". Abujjahali baada ya kusikiliza maelezo hayo hakuwa na la kusema ila kucheka tu na kumdhihaki. Alithubutu kusema kwamba Muhammad (saw) alikuwa muongo, kwa sababu haiwezekani usiku mmoja aende hadi mbinguni.

"Ninaona uongo wako umetia fora sasa, khabari za mbingu na Arshi si mchezo wala hatuwezi kuzihisi. Tuambiye hali ya Baitul-Mukaddasi kwa sababu huko tumepata kwenda, tunajuwa alama zake", alisema Abujjahali kumwambia Mtume (saw). Basi, Mtume (saw) akaingiwa na khofu moyoni mwake kwa nini mambo ya usiku ule asiweze kuyapambanuwa. Allah Akamuamuru Jibril anakili mambo yote yalivyo na kuyawakilisha kwake. AbuBakari na Makureshi wengine, waliafikiyana na Mtume (saw) juu ya safari yake hiyo. Bali wao nao walimuuliza kwa kumwambia wao wana watu wao Bani fulani, je hao wangefika lini hasa pale Makka! Walitaka kufahamu. Mtume (saw) akawajibu na kuwaambia kwamba watu hao hawapo mbali sana nao wangefika pale siku ya Ijumaa ya tano kuanzia siku ile. Naam, siku ilipotimu, wale watu wakafika kama alivyoarifu Mtume (saw). Wale Makureishi wakasema kumwambia Mtume (saw) kwamba maelezo yake yalikuwa sahihi kabisa. Pamoja na hayo, wao lakini hawapo twayari kuacha masanamu yao wakamfuata yeye!

Basi Mtukufu Mtume Muhammad (saw) tangu siku ile aliyokwenda mbinguni, mwili wake ulikuwa unanukia harufu nzuri ya mbinguni. Harufu nzuri ya miski. KIla mahali apitapo, watu walikuwa wanatambuwa kwamba hapo kapita Mjumbe wa Allah, Mtukufu Mtume Muhammad. Hapa ndipo mwisho wa safari ya mbali.

MIIRAJI:
Kuna maelezo mbalimbali ya wanazuoni yanayozungumziya kuhusu uhakika hasa wa kisa cha safari hii ya Miiraji. Kuna wanaoamini kwamba Mtume (saw) alifanya safari hii kimwili. Wanatilia uzito wa maelezo yao kwa kauli inayosema Mwenyezi Mungu Anao uwezo wa kuupitisha mwili wa Muhammad (saw) sehemu zile zote zilizotajwa katika msafara huu. Kwao hao tunayo maswali mengi ya kuwauliza. Bali mimi hapa nitayawasilisha kwa wanazuoni hao kupitia kwenu wasomaji wangu wapenzi wa makala haya. Bali soma kisa chenyewe mara mbili tatu katika kila hatuwa, haikosi utajiuliza. Ni kweli kabisa kwamba Mwenyezi Mungu Ana uwezo wa kufanya chochote Apendacho. Lakini Mwenyewe kajiwekea taratibu na wala hazivunji kamwe. Naye Ametuambia kuwa hatutakuta mabadiliko yoyote katika taratibu zake. Sisi wanadamu, wanyama, ndege na wadudu mbalimbali tumepangiwa kuzaliwa, kuishi na kufa hapa hapa duniani. Utaratibu ambao Mwenyezi Mungu Ameuweka tangu azali wala hajauvunja hata siku moja. Sasa niwaulize maswali:-

1. Opasuaji (Operation) aliyofanyiwa Mtume (saw) ilifanyiwa nyumbani kwake. Je bibi Aisha aliona shughuli hiyo ikifanywa?

2. Buraku alizungumza na Muhammad (saw). Je, kwa lugha na kwa sauti ya binadamu, mnyama au ndege?

3. Mtume Muhammad (saw) aliona umbo lote la Nabii Musa (as) hadi ini la nyama, je wale Manabii wengine hali ilikuwaje? Jicho halikuona vyema?

4. Katika kila uwingu, Jibril na Muhammad (saw) walipofika, mabawabu walikuwa wanaambiwa wafunguwe milango, je mbingu hadi mbingu kuna kizuizi kati?

5. Kama safari hii ilikuwa ya kiwiliwili, wale Mabii wa zamani aliwaswalisha katika hali gani? Je walifufuliwa na kuvishwa mwili mpya kabla ya siku ya kiyama?

6. Tumesimuliwa kwamba Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alipoingia kwenye hijabu, hapo akamuona Mwenyezi Mungu ana kwa ana. Alimuona kwa mboni ya macho yake mawili. Qur'an bali Uislam kwa ujumla unatufundisha kwamba Allah Haonekani kwa macho yetu haya. Macho haya hayamfikii Mwenyezi Mungu, bali Yeye Anayafikia hayo macho. Seyidna Musa (as) aliomba sana ili amuone Allah ana kwa ana, lakini hilo halikuwezekana, bali alioneshwa Ishara mbadala kuwapo kwake Mwenyezi Mungu. Hiyo ilitosha kwa Seyidna Musa (as) kumhakikishia kuwapo kwa Mungu. Kwa Mtume Muhammad (saw) je imekuwaje hivyo?

Ukweli halisi wa safari ya Miiraji ya Mtume wetu Muhammad (saw) ilikuwa ya kiroho wala si ya kimwili. "Utukufu ni wa Yeye Ambaye Alimpeleka Mtumishi wake usiku kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa mbali ambao Tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake, ili Tumwonyeshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Asikiaye Aonaye". Qur'an Tukufu sura 17 aya ya pili. "Na (kumbuka) Tulipokuambia: Hakika Mola wako Amewazunguka watu. Na Hatukuifanya njozi ile Tuliyokuonyesha ila kwa kuwajaribu watu na (pia) mti uliolaaniwa katika Qur'an. Na Tunawahadharisha, lakini haiwazidishii ila uasi mkubwa" (17:61). **-Mwisho-**

Ukweli wa Ahmadiyya wadhihirika mjini Mbinga

Kutoka uk. 12

abii hawajafariki.

Baada ya majibu hayo wakatangaza kwamba hivi sasa muda umekwisha tutaendelea kesho, wakasema kesho watakuja kuthibitisha uhai wa Nabii Issa (as) pamoja na baadhi ya Manabii. Kesho yake yaani th.28/04/2012 mimi (Mwalimu Kaisi Alli) nililazimika kuondoka kwenda Mbinga kuungana na Mwalimu mwenzangu yaani Mwl. Iddi Issa kwa ajili ya kujibu mashambulizi dhidi ya Ahmadiyya.

Muda wa mjadala ulifika saa tisa jioni, mimi (Mwl. Kaisi Alli) na Mwalimu Iddi Issa tulifika mapema kwenye mjadala, cha ajabu ni kwamba baadhi ya wale wahadihiri wa Kisunni waliponiona walianza kugwaya kwa sababu wananifahamu sana tena baadhi yao ni marafiki zangu kwa mfano Ustadhi Salimu Mbaya Kitete huyu ni rafiki yangu wa miaka mingi na afahamu hoja za Ahmadiyya, hivyo waliponiona ghafla pale Mbinga walishtuka kwa sababu hawakutarajia kama mimi ningeweza kufika pale Mbinga kwa haraka sana, kwa sababu hawa wahadhiri mimi nilishawahi kukutana nao kwenye mjadala mwingine mjini Songea, wakashindwa vibaya kwenye hoja ya Yesu kuoa hivyo waliponiona walijua kwamba wangepata fedheha nyingine mbele ya umati wa watu.

Wakati wa kuwasilisha mada uliwadia Mwalimu Iddi Issa aliwasilisha mada kwa kunukuu aya ile ile aliyoinukuu jana yake yaani sura ya 3:145.

Ilipofika zamu ya wahadhiri wa Kisunni kujibu hoja Bw. Gelemanus Jamal ambaye kwa asili alikuwa ni Mkristo aliyesilimu hivi karibuni ambaye hafahamu vizuri maneno ya Kurani Tukufu na sawa na maelezo ya watu waliofika pale wanasema kwamba yule Bw. Gelemanus Jamal hafahamu kabisa kusoma maneno ya Kurani Tukufu, yeye Bw. Gelemanus ndiye alikuwa mtu wa kwanza kum zigo la kujibu hoja za Ahmadiyya. Bwana huyu alianza kujibu hoja akinukuu sura ya 4:157 - 158 kwa mujibu wa tafsiri ya Sheikh Abdallah Saleh Farsy inayosema kwamba Nabii Issa (as) hakuuawa na wala hawakumtesa pale msalabani bali aliyeteswa ni mtu mwingine. Aliendelea kutoa maelezo kwamba Nabii Issa (as) alipaishwa mbinguni mzima mzima na mwili wake na hivi sasa yupo mkono wa kuume wa Mungu.
Ndipo Mhadhiri wa Ahmadiyya Mwl. Kaisi Alli aliposimama na kuanza kumdodosa Bw. Gelemanus kulingana na tafsiri ya aya alizozisoma. Mwalimu Kais alieleza kuwa aya zilizosomwa na Bw. Gelemanus hazionyeshi kabisa kwamba Nabii Issa (as) yupo hai mbinguni, bali aya hizo zinatoa habari ambapo Mwenyezi Mungu Anakanusha kauli ya Mayahudi inayosema kwamba eti wamemwua Nabii wa Mungu Nabii Issa (as) katika msalaba hali hawakumwua kwa kifo chochote na wala ule msalaba haukusababisha kifo kwa Nabii Issa (as) Nabii wa Mungu ingawa kweli alifikishwa pale msalabani na kupata mateso, lakini hatimaye Mwenyezi Mungu alimuepusha na kifo kile cha laana cha msalaba bali Mwenyezi Mungu Alimnyanyua kwake au kwa maneno mengine Mwenyezi Mungu Alimtakasa Nabii Issa (as) kutokana na kifo kile cha laana walichokusudia Mayahudi kumuua.

Baada ya maelezo hayo ya Mwalimu Kais Alli ndipo Bw. Gelemanus alijitutumua akitaka kupinga hoja na maelezo hayo ya Mwalimu wa Ahmadiyya, yeye alisema kwamba maelezo hayo sio ya kweli bali Nabii Issa (as) hakuwahi kufikishwa hata pale msalabani bali aliyefikishwa pale msalabani ni mtu mwingine, ingawa hakumtaja mtu huyo alikuwa nani. Bwana Gelemanus aliendelea na hoja ya kuwa neno "SWALAB" lililotumika katika aya ya 4:157) maana yake ni kutesa hivyo Nabii Issa (as) hakuteswa pale msalabani.

Bwana huyu alisisitiza sana hoja yake hiyo licha ya kuwa wahadhiri wa Ahmadiyya walitoa ufafanuzi wa kina kuhusu tafsiri ya neno hilo "SWALAB" kwamba neno hilo halina maana ya mtu kumtesa msalabani , bali maana

yake sahihi ni mtu kuwekwa msalabani na afie pale msalabani na kuvunjwa miguu yake ndipo neno "Swalab" linapotimia, sio kuwekwa tu msalabani pasipo kifo kutimia. Hivyo basi kwa Nabii Issa (as) mambo hayo yote mawili hayakufanyika, yaani Mayahudi hawakumwua Nabii Issa (as) kwa kifo chochote wala hawakumvunja miguu yake ingawa alipata mateso ya kufikishwa pale msalabani.

Bw. Gelemanus alikuwa mgumu wa kuelewa kiasi ambacho aliomba ushahidi wa maandiko kuhusiana na maelezo hayo. Ndipo alipopewa ushahidi wa maneno ya Kurani Tukufu kutoka aya 12:42 inayosema kwamba "Enyi wafungwa wenzangu wawili, ama mmoja wenu atamnywesha Bwana wake pombe, na ama mwingine basi atauawa kwa kusulubiwa, ..." hivyo basi kwa maelezo ya aya hiyo hapo juu neno "SWALAB" maana yake ni kuuawa katika msalaba, sio kutesa katika msalaba tu, hivyo basi Nabii Issa (as) aliteseka katika msalaba bali hakuuawa katika msalaba ule.

Baada ya maelezo hayo Bwana Gelemanus akaona unga umejaa maji hakuweza kuendelea tena na hoja akaamua kuondoka na kumpisha mwenzake ili aje kunusuru jahazi lao lililokuwa linaelekea kuzama, ndipo alipokuja muhadhiri mwingine wa Kisunni. Ingawa huyu alionekana ni Answar Sunna kwa mujibu wa mavazi yake ya suruali ya njiwa na kanzu yake pia ilikuwa ni staili hiyohiyo ya njiwa.



Sawa na ushahidi wa midomo na maandishi kutoka kwa watu mashuhuri wa Srinagar, Kashmir, aliyezikwa katika kaburi hili ni Nabii aitwaye Yus Asaf ambaye pia aliitwa Mwanamfalme, aliyefika Kashmir miaka 2000 iliyopita.

Ndipo alianza kwa mbwembwe nyingi na kujifanya kuwa anajua lugha ya kiarabu. Yeye alisema kuwa ndani ya Kurani Tukufu Mwenyezi Mungu Anasema kuwa "BAL RAFAAHULLAHU ILAIHI" yaani Bali Mwenyezi Mungu Alimnyanyua (Nabii Issa as) kwake 4:158. Akaendelea kueleza kwamba kwa mujibu wa aya hiyo hapo juu ni wazi kwamba Nabii Issa (as) amenyanyuliwa na kwamba sasa yupo mbinguni kwa Mwenyezi Mungu.

Ndipo ilipofika zamu ya Ahmadiyya kutoa maelezo juu ya hoja hiyo. Mwl. Kaisi Alli akajibu hoja kwa kusema kwamba kwa kuwa inaonekana tatizo linalowatatiza katika aya hiyo ni neno "RAFAA" - yaani kunyanyua. Hivyo Mwalimu Kais alisoma aya ya 3:56 ya Kurani Tukufu inayosema kuwa "IDH KAALA LLAHU YAA ISSA INNI MUTAWAFFIIKA WA RAAFIUKA ILAIYA" - yaani Mwenyezi Mungu Aliposema, Ewe Issa, kwa yakini Mimi Nitakufisha na Nitakuinua Kwangu. Kwa mujibu wa aya hiyo na kwa kulingana na mtiririko wa maneno katika aya hiyo ni kwamba Nabii Issa (as) kwanza atafishwa ndipo kisha atanyanyuliwa kwa Mwenyezi Mungu na ndivyo ilivyo kwa roho zote za watu kwamba wakishafariki zinakwenda kwa Mwenyezi Mungu. Mwalimu Kais aliendelea kueleza kwamba neno "TAWAFFA" kufisha lililotumika katika aya hiyo haina maana nyingine isipokuwa ni kufisha tu, kwa sababu Mwenyezi Mungu Amelitumia neno hilo "TAWAFFA" mara nyingi ndani ya Kurani Tukufu kwa maana ya kifo kwa mfano sura 2:235, 5:118, 7:38, 4:98, n.k).

Baada ya maelezo hayo mhadhiri wa Kisunni alipinga maelezo hayo akisema kwamba neno (Tawaffa) halina maana peke yake kwamba ni kifo tu, bali maana nyingine ni (Kulipwa ujira) alinukuu aya ya sura ya 3:186 inayosema kwamba "Kila nafsi itaonja mauti, na bila shaka mtapewa ujira wenu sawa sawa siku ya kiyama".

Mwalimu Kaisi -mhadhiri wa Ahmadiyya alieleza kwamba kwa mujibu wa aya hiyo ujira mtu atapewa baada ya kifo siku ya kiyama, hivyo neno 'Tawaffa' maana yake bado inaendelea kuwa ni kifo.

Kufikia hapo jahazi la wahadhiri wa Kisunni likawa limetota na kuzama kabisa, wakawa hawana hoja tena. Kama inavyofahamika kwamba katika mji wa Mbinga asilimia 99 ya watu wake ni ndugu zetu Waktisto baada ya kuona wahadhiri wa Kisunni wameshindwa kujibu hoja za Ahmadiyya walianza kuwashangilia Wahadhiri wa Ahmadiyy kama vile ushindani wa mpira wa yanga na simba. Kitendo kile cha kuwashangilia Waahmadiyya kiliwaudhi sana Wahadhiri wa Kisunni kiasi ambacho wakaanza kuwabembeleza ndugu zetu Wakristo kwa kusema kwamba wasiwashangilie Waahmadiyy kwa sababu eti wao (Waahmadiyya) wanasema Nabii Issa (as) ambaye ni Yesu Kristo amekufa hayupo mbinguni na kaburi lake lipo India, wakati sisi (Wasunni) tunasema Yesu hakufa bali yupo mbinguni kama mnavyoamini nyinyi Wakristo, sasa hamuoni kwamba nyinyi (Wakristo) na sisi (Wasunni) ni kitu kimoja?

Baada ya maelezo hayo yaliyotamkwa hapo juu na Bwana Mikidadi ambaye ndiye alikuwa ni Mwenyekiti wa muhadhara ule, ndugu zetu Wakristo walishangia sana tena kwa nguvu zaidi kwa kuona kwamba kumbe wao na Wasunni ni kitu kimoja. Baada ya hapo Bw. Mikidadi Mwenyekiti wa mhadhara ule alitangaza mbele ya umati ule kuwafukuza wahadhiri wa Ahmadiyya kwenye muhadhara ule akisema ya kwamba Waahmadiyya wanavuruga mhadhara wao. Baada ya kutamka maneno hayo ndugu zetu Wakristo wakalipuka tena kuwashangilia Waahmadiyya huku wakiimba kuwa Ahmadiyya ni vidume.

Ndugu wasomaji wapendwa mmeshaona jinsi ndugu zetu hawa wahadhiri wa Kisunni walivyokuwa na imani dhahifu ya kumfanya Nabii Issa awe hai huko mbinguni inawafanya ndugu zetu Wakristo washangilie na waamini kwamba kumbe dini yao bado ni hai kwa sababu Nabii wao Yesu bado yupo hai huko mbinguni. Ilhali kuendelea kuamini hivyo ni kuendelea kuthibitissha kwamba kumbe inawezekana Yesu akawa ni mtoto mpendwa wa Mungu kuliko Manabii wengine. Hivyo basi ndugu zangu Waislam jaribuni kujifikiria kuhusiana na imani hiyo, kwa sababu inamvunjia heshima Mwenyezi Mungu na Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ambaye ni mkubwa wa Manabii na ni Mbora wa Manabii wote. Kwa hiyo imani hiyo ni ya kishirikina ambapo Waislam wameepukana na ushirikina

Tarehe 29/04/2012 mimi (Mwalimu Kais) pamoja na Mwalimu Iddi Issa tulikwenda tena kwenye ule mhadhara kwa nia ya kutaka kuuliza maswali, lakini kwa mshangao mkubwa walitangaza mbele ya watu kwamba Waahmadiyya hatutawapa kipaza sauti ili waongee. Kitendo hicho cha kuwakatalia Waahmadiyya kuongea, kiliamsha shangwe tena kwa ndugu zetu Wakristo wakiimba kwamba Waahmadiyya ni vidume.

Hivyo ndugu zangu wasomaji wapendwa kuhusiana na hoja hiyo ya kifo cha Nabii Issa (as) hakuna shaka kuwa Nabii Issa amekwisha fariki kifo cha kawaida na kaburi lake lipo India katika jimbo la Kashmir mtaa wa Khanyar Srinagar. Mwenye masikio na asikie, kwani hatarudi tena duniani kama inavyodhaniwa na ndugu zetu walio wengi wa Kisuni na Wakristo.

Mwisho namalizia maneno ya mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as), alisema kwamba; "Kumbukeni ya kwamba hakuna atakayeshuka toka mbinguni, wapinzani wetu wote waliopo hivi sasa watakufa na hakuna mmojawapo atakayemuona Yesu mwana wa Mariam akiteremka kutoka mbingini, baadaye Wazao wao watowarithisha pia watakufa bila ya hata mmoja wao atakayemuona Yesu mwana wa Mariam akishuka toka mbinguni. Kadhalika watoto wa wazao wao nao watakufa bila kumwona mwana wa Mariam akiteremka kutoka mbinguni, hapo Mwenyezi Mungu Atatia wasiwasi mioyoni mwao ya kwamba siku za utukufu wa msalaba tayari zimepita na dunia imeingia katika hatua mpya, ilihali mwana wa Mariam bado hayashuka toka mbinguni, na hapo wale wenye busara miongoni mwao wataitupilia mbali imani hii wote kwa pamoja. NA KUANZIA HII LEO KARNE YA TATU HAITAKUWA IMEPITA, ambapo wale wamgojeao Yesu haidhuru wawe Wakristo au Waislam, wataudhika na kuiacha imani hii mbovu. Na kutabakia na dini moja na kongozi mmoja tu. Mimi nimekuja kupanda mbegu, mbegu tayari nimeipanda kwa mkono wangu, sasa itamea na kukua na kustawi, hakuna awezaye kuizuia" (Tadhkiratul Shahadataini Uk.65 Octoba mwaka 1903).

-Mwisho-

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

Mapenzi ya Mungu

Ramadhan 1433 AH | Agosti 2012 | Zahoor 1391 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Safina r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Ukhalifa utakuwa kwa miaka thelathini. Kisha baadaye ufalme utapatikana .... (*Musnad Ahmad*)

Ukweli wa Ahmadiyya wadhihirika mjini Mbinga,

Wahadhiri wa Kisunni waumbuka; Washindwa kujibu hoja za Ahmadiyya

Na Mwl. Kaisi Alli - Mkongotema Songea.

Umati mkubwa wa watu akina baba na akina mama, watoto na vijana, ulikusanyika katika soko kuu la wilaya ya mbinga, umati huu ulishuhudia maajabu ya mwaka walipo waona wahadhiri wa Kisunni waliposhindwa vibaya sana tena kwa aibu kubwa kujibu hoja za wahadhiri wa Ahmadiyya.

Tarehe 28/04/2012 ulifanyika mjadala mkubwa kati ya Wahadhiri wa Ahmadiyya na Wahadhiri wa Kisunni, mjadala huu ulifanyika katika maeneo ya soko kuu la Wilaya ya Mbinga (Mjini). Mada iliyokuwa inazungumzwa ni "Kifo cha Nabii Issa (as)". Umati mkubwa wa watu ulikusanyika, inakadiriwa zaidi ya watu 3000 ili kushuhudia yatakayojiri katika mjadala huo.

Wazungumzaji upande wa Kissunni baadhi yao ni hawa wafuatao: - Bw. Salimu Mbaya Kitete, Ustadhi Issa Mbamba, Bw. Misanya, Bw. Gelemanus Jamal na Bw. Mikidadi. Na kwa upande wa Ahmadiyya wazungumzaji walikuwa ni Mwl. Iddi Issa wa Jamaat ya Mbinga Mjini na Mwl. Kaisi Alli ambaye ni mwandishiw a makala hii, yeye ni mwalimu wa Jamaat ya Mkongotema - Madaba, Songea.



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s , Masihi Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

Mjadala huo ulianza saa tisa jioni, itakumbukwa kwamba mjadala huo ulianza jana yake yaani th.27/04/2012, ambapo Mkristo mmoja Bw. Kaumeme aliuliza swali kwa wahadhiri wa Kisunni kwamba kuna baadhi ya Waislam - Ahmadiyya wanasema kwamba Nabii Issa (as) amefariki, je nyinyi Masheikh wa Kisunni mnasemaje kuhusiana na hoja hiyo?

Majibu kwa wahadhiri wa Kisunni ni kama ifuatavyo; Hao Makadiani ni waongo tena ni makafiri wakubwa sana na ni wapinzani wa aya za Mwenyezi Mungu hao Makadiani msiwasikilize ni waongo.

Baada ya majibu haya ndugu zetu wasamaria wema walipeleka habari hiyo kwa Mwalimu wetu wa Jamaat ya Mbinga Mwalimu Iddi Issa naye bila ajizi aliwafuata wale wahadhiri wa Kisunni kwenda kuwajibu, ifahamike kwamba hawa Wasunni walikuwa na mhadhara wao katika maeneo haya ya soko kuu la Wilaya ya Mbinga.

Mwalimu Iddi Issa alifika katika viwanja vya mhadhara akaomba nafasi ya kuongea akakaribishwa. Akaanza kueleza kwamba nimekuja kujibu hoja iliyoelezwa jana kwamba eti Waahmadiyya ni makafiri na waongo eti kwa sababu wanaamini na kusema kwamba Nabii Issa (as) amefariki,. Mwalimu Iddi Issa aliendelea kusema kwamba kwa mujibu wa maneno ya Mwenyezi Mungu ya Kurani Tukufu sura ya 3:145 inasema kwamba; "Na siye Muhammad ila yu Mtume, bila shaka wamekwishafariki kabla yake Mitume .....". Kwa mujibu wa aya hii Mwalimu Iddi Issa aliendelea kuitolea maelezo kwamba Mitume wote ambao walikuja kabla ya Mtume Muhammad (saw) wamekwisha fariki akiwemo pamoja na Nabii Issa (as) ambaye alikuja kabla ya Mtume Muhammad (saw).

Ilifika zamu ya wahadhiri wa Kissunni kujibu hoja wote kwa pamoja wahadhiri wa Kissuni walikubali kwamba kwa mujibu wa aya hiyo ni kweli Manabii wote waliokuja kabla ya Mtume Muhammad (saw) wamefariki isipokuwa kuna baadhi ya Man-

Endelea uk. 11

Falsafa ya safari ya Mbali - Miiraj

Na Ustadh Khamisi Wamwera, Mbagara rangi 3 Dar es salaam



Al Ustadh Khamis Wamwera

Hapo pia hakuweza kukaa sana, mara wakaandoka kuelekea mbingu ya nne. Walipofika Seyidna Jibril aliwaambia mabawabu wafunguwe milango kwa sababu Mtume (saw) anataka kuingia ndani. Mabawabu nao wakasema, "Sawa, haya pita naye". Walipoingia wakalakiwa na Nabii Idrisa. Baada ya hapo, Jibril na Muhammad (saw) waliingia uwingu wa tano. Huko walikutana na Nabii Haruni ambaye aliwakaribu vizuri sana. Wote wakaomba dua kwa Allah tena pamoja kwa niya moja tu kwamba MwenyeziMunguAwabarikiye. Kisha Mtume Muhammad (saw) na Jibril walifika mbingu ya sita. Wakapiga hodi langoni kwa tabajuli. Wakafunguliwa taratibu kabisa. Hapa walikutana na Nabii Musa (as) ambaye ndiye Kalima llah. Vile vile hapo waliona jeshi kubwa likimlinda Seyidna Musa. Jibril akamwambia Muhammad (saw), "Hebu inua kichwa chako utazame mambo". Naam, ni mambo kweli. Aliona kundi kubwa la jeshi ambalo halioneshi mwanzo wala mwisho wake. Jibril akasema kwa Muhammad (saw) kwamba lile jeshi analoliona ni lake lote. Kisha Seyidna Musa alionekana umbo lake lote hadi ini la nyama. Seyidna Musa alikuwa na nywele nyingi zilizosimama za tomatoma.

Katika hali hiyo, Mtukufu Mtume Muhammad (saw) akamtolea salaam Nabii Musa (as), Nabii Musa akaitikia kisha akamkaribisha vyema sana. Musa akamwambia Muhammad (saw), "Ewe ndiwe muombezi wa watu wote, kwa hiyo utakapofika kwa Mwenyezi Mungu, tafadhali nasi utukumbuke kwa maombi".

Toka hapo, Jibril na Mtume Muhammad (saw) wakaingia mbingu ya saba. Seyidna Jibril kwa adabu na taadhima, akatamka pale mlangoni pa Mabawabu hivi, "Jamani, nimekuja naye Habibu Seyidna Muhammad Mustafa, tafadhali funguweni mlango ili Mtume wa Mungu aweze kuingia ndani". Mara lango likafunguliwa na Mjumbe wa Allah akapita. Hapo Mtume (saw) akamuona Mtume mwenye sura iliyojaa nuru na jaha kuu. Mtume (saw) akamuuliza JIbril, yule alikuwa mtu gani. Seyidna Jibril akamjibu kwamba huyo ndiye Seyidna Ibrahimu Khalilullah. Seyidna Muhammad (saw) akamtolea salaam na Mzee Ibrahimu akaitikia na kumkaribisha vizuri. Kisha Mzee Ibrahimu akamkong'otea Muhammad (saw) na kumwambia "Jaha ni yako ewe muombezi wa ulimwengu. Nakuomba uwaambiye watu wa umati wako waweke mbeko na wachukue masurufu mema ya akhera"

Pale walipokuwapo vile vile palionekana watu weupe kwelikweli. Weupe wake ni kama karatasi. Mtume (saw) akastaajabu sana kisha aliuliza hao walikuwa watu gani. Seyidna Jibril akajibu akamwambia hao ni watu wema ambao hawatendi mambo maovu na mabaya.

Walipotoka hapo, Seyidna Jibril na Mtume Mummad (saw) wakaingia Baitul-Maamuri ambayo ipo chini ya pepo. Baitul-Maamuri imezungukwa na walinzi malaika. Wakaingia humo. Wakati wa swala ulifika, Seyidna Jibril akatowa adhana. Kwa hapa swala iliongozwa na malaika Mikaili ndiye alikuwa Imamu. Hiyo ilikuwa siku ya Ijumaa, ambapo waliweza kuswali rakaa mbili. Baada ya swala, wote kwa pamoja waliendelea kwa uradi kumuomba Mwenyezi Mungu zaidi. Mtume Muhammad (saw) aliwaombeya waaminio wote. Malaika Mikaili akashufaiya pamoja na malaika wengine ambao walikuwa maamuma wakakazia maombi kwa Mwenyezi Mungu.

Kutoka hapo ndipo wakaona ARSHI, kile kiti cha Enzi. Jibril na Mtume (saw) wakakiendea. Hapo ndipo paitwapo SIDIRATUL-MUNTANA. Wakaona mambo mengi ya ajabu ajabu. Chini ya kiti hicho waliona mito minne inatiririka. Mmoja ulikuwa wa maji, wa pili ulikuwa wa maziwa, wa tatu ulikuwa wa asali na wa nne ulikuwa wa khamri.

Kilizungukwa na mikunazi. Kunazi zake zilikuwa tamu mno kama au zaidi ya sukari na asali. Jani moja la mikunazi hiyo, iliweza kuwafunika watu wengi mno. Upana wa jani moja

Endelea uk. 10